**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA WA 2025/2026

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHE. SHAMATA SHAAME KHAMIS (MBM)**
**WAZIRI WA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO**
**ZANZIBAR**

**MEI, 2025**

## YALIYOMO

UTANGULIZI ..... 1

MUUNDO NA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO. ..... 4
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI 2025 ..... 5
Mapato Yaliyokusanywa Kulingana na Malengo Yaliyowekwa ..... 5
Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji ..... 5
Fedha Iliyopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji ..... 9

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI 2025. ..... 9
PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO ..... 11
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji ..... 11
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula. ..... 12
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ..... 13
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar – ZALIRI ..... 13

PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU ..... 14
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO ..... 15
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo ..... 15
PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO ..... 16
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..... 16
Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..... 17
Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba ..... 17

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ..... 18
Makadirio ya Mapato ..... 18
Makadirio ya Matumizi 2025/2026 ..... 18

MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026. ..... 18
PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO ..... 19
Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji ..... 19
Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula ..... 20
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar (ZALIRI). ..... 20
Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ..... 21
PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU ..... 21
PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO ..... 22
Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo ..... 22

PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO ..... 23
Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..... 23
Mipango, Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ..... 23
Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba ..... 24

MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ..... 24
SHUKURANI ..... 24

VIAMBATANISHO ..... 27

Kiambatanisho Nam. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2023 -2024, Zanzibar ..... 27
Kiambatanisho Nam. 2A: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchinjwa, 2024 ..... 28
Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2024 ..... 29
Kiambatanisho Nam. 2C: Idadi ya Wanyama Wengine waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2024. ..... 30
Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2024. ..... 31
Kiambatanisho Nam. 4: Ukusanyaji wa Mapato, Julai 2024 - Machi 2025 ..... 32
Kiambatanisho Nam. 5: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2024 Hadi Machi, 2025. ..... 33
Kiambatanisho Nam. 6A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 ..... 34
Kiambatanisho Nam. 6B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026. ..... 35
Kiambatanisho Nam. 7A: Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji ..... 37
Kiambatanisho Nam 7B: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula ..... 38
Kiambatanisho Nam 7C: Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi (Kaskaizini Unguja na Kaskazini Pemba) ..... 39
Kiambatanisho Nam. 7D: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R ..... 41
Kiambatanisho Nam. 7E: Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji ..... 43
Kiambatanisho Nam. 7F: Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Hifadhi ya Akiba ya Ufufuma-Pongwe ..... 44
Kiambatanisho Nam. 7G: Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC) 45
Kiambatanisho Nam. 7H: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu ..... 47
Kiambatanisho Nam. 7I: Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha usalama wa chakula (STREPHIT) ..... 49
Kiambatanisho Nam. 7J: Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR ..... 51
Kiambatanisho Nam. 7K: Mradi wa Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unaozingatia Mabadiliko ya Tabianchi ..... 52
Kiambatanisho Nam 7L: Mradi wa Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Huduma Endelevu za Ugani wa Kilimo ..... 53
Kiambatanisho Nam 7M: Mradi wa Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakbali wa Sekta ya Kilimo ..... 54

Kiambatanisho Nam 7N: Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanic garden) na Mashamba ya Serikali ....................................................................................................55
Kiambatanisho Nam. 8: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2025/2026 ......56

## HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026, ambayo yanawasilishwa katika mfumo wa Programu (PBB). Aidha, bajeti hii ni bajeti inayozingatia jinsia (GRB), hasa tukizingatia kwamba inakusudia kutekeleza **'Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo'** unaotilia mkazo ushiriki wa vijana na wanawake kuwaondosha katika kilimo cha kujikimu kuelekea '**KILIMO BIASHARA'**.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuwa na amani, utulivu na kutuwezesha kufikia leo tukiwa wazima na wenye afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambapo inakadiriwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wake wanajihusisha na kazi za kilimo, ufugaji na uhifadhi wa maliasili.

3. **Mheshimiwa Spika,** pili napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 kwa kuvuka malengo. Vile vile, napenda kumpongeza Mhe. Rais kwa kupitishwa na Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa nafasi ya Uras katika uchaguzi ujao wa Oktoba 2025 - **HONGERA SANA Mh. Rais.**

4. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuingoza na kuisimamia Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa kipindi chote hiki. Halikadhalika, nnamuhakikishia kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu na naahidi kwamba nitaitumikia Serikali hii kwa uwezo wangu wote kwa kutekeleza kwa vitendo ILANI ya Uchaguzi ya CCM ili kuleta mageuzi katika sekta ya Kilimo nchini.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kumshauri vizuri Mhe. Rais katika kuendeleza sekta ya kilimo. Ninawashukuru kwa maelekezo na miongozo yao wanayoitoa kwa sekta ya kilimo kwa kadri inavyohitajika.

6. **Mheshimiwa Spika,** nakupongeza wewe binafsi kwa umakini na umahiri wako wa kuliongoza na kulisimamia Baraza la Wawakilishi, pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi wanaokusaidia katika kazi hizo na

tunawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu awarudishe tena, nyote, kipindi kijacho ili murudi kuendeleza uwezo, hekima na busara katika kuliendesha Baraza kwa ufanisi, kasi na mafanikio zaidi.

7. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Utalii, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Bumbwini pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii kwa ushauri na miongozo wanayoitoa kwa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo katika kufanikisha utekelezaji wa malengo kwenye bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/2025. Aidha, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma Mwakilishi wa Wananchi wa jimbo la Dimani, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2025/2026. Napenda kukuhakikishia kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo waliyotupatia tumeyazingatia na kuyaweka katika bajeti hii ninayoiwasilisha.

8. **Mheshimiwa Spika,** mwisho, lakini sio kwa umuhimu, natumia nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Micheweni kwa kunipa mashirikiano na kuwa pamoja nami katika suala zima la kufanikisha maendeleo ya jimbo letu na nchi kwa ujumla. Naahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta tija na maendeleo jimboni mwetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo inaendeleza Mipango na Mikakati iliyoanzishwa na Serikali katika kuendeleza Sekta hii ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inapunguza utegemezi wa mahitaji ya chakula; kwa kuendeleza kilimo biashara katika uzalishaji wa mazao ya chakula na kuwawezesha vijana kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Juhudi nyengine ni kuimarisha uzalishaji wa mazao ya viungo, mboga na matunda pamoja na mazao ya mizizi ambayo ndio chachu ya maendeleo katika sekta za utalii na viwanda na kuendeleza uzalishaji wa zao la nazi na karafuu. Vilevile, upatikanaji mzuri wa huduma za mifugo ikiwemo dawa, chanjo na utoaji wa elimu juu ya ufugaji, uzalishaji wenye tija na matumizi ya mbegu bora za mifugo utaendelezwa. Kadhalika, Wizara hii itaendelea na usimamizi wa rasilimali za misitu ya hifadhi na ya jamii kwa lengo la kuhifadhi bioanuai, mazingira pamoja na kuimarisha huduma za utalii wa kimaumbile.

10. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inayojumuisha mazao, mifugo na maliasili za misitu bado ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar, ambapo inatoa mchango mkubwa kwa wananchi kujikimu kimaisha. Sekta hii inaajiri takriban asilimia 35 ya wananchi wa Zanzibar na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 wanaitegemea katika kujikimu kimaisha. Lengo kuu la Wizara ni kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji kwa kutumia mbinu bora na teknolojia za kisasa, upatikanaji wa masoko na hatimae kukuza

pato la Taifa sambamba na uhifadhi wa maliasili zetu. Kwa mwaka 2024, Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 24.3 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 24.9 iliyoripotiwa mwaka 2023. Hii inaonesha kuimarika kwa sekta nyengine zinazohudumiwa na sekta ya kilimo na ni alama nzuri kwa uchumi wetu.

11. **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kwamba jumla ya eneo lililopandwa mazao ya kilimo kwa mwaka 2024 limepungua hadi kufikia ekari 104,667.8 ikilinganishwa na ekari 122,514.2 za mwaka 2023, sawa na upungufu wa ekari 17,846.4 Kati ya eneo hilo, ekari 81,402.9 ambazo ni sawa na asilimia 78 zilipandwa mazao ya chakula. Zao la mpunga lilipandwa katika eneo la ekari 30,315.2 ambazo ni sawa na asilimia 29 ya eneo lote lilopandwa mazao kwa mwaka 2024, zao la muhogo lilipandwa katika eneo la ekari 20,080.4 ambazo ni sawa na asilimia 19, na zao la ndizi lilipandwa katika eneo la ekari 7,303.3 ambazo ni sawa na asilimia 7 (**Kiambatanisho Nam. 1**). Hivyo, Wizara inaendelea na juhudi za kuhamasisha wakulima kulima mazao ya chakula, mboga, matunda na viungo ili kutosheleza soko la ndani likiwemo la utalii sambamba na kuongeza pato la Taifa.

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya kilimo umepungua kwa tofauti ya tani 144,870.8 kutoka tani 527,800 mwaka 2023 ikilinganishwa na tani 382,929.2 mwaka 2024. Upungufu huo umetokana na kuwepo kwa vipindi virefu vya mvua na jua visivyotabirika. Wizara imekuwa ikifanya jitihada za kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji toka mwaka 2017, ambapo hadi sasa eneo lililowekewa miundombinu ya umwagiliaji limefikia ekari 5,750 (sawa na hekta 2,300). Kutokana na uimarishaji huo natija ya uzalishaji kwa mpunga wa umwagiliaji kwa mwaka 2024 imeongezeka kutoka tani 1.857 hadi tani 2.023 kwa ekari ambayo imepelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa mpunga wa umwagiliaji kutoka tani 7,296.5 mwaka 2023 hadi kufikia tani 11,634.5 mwaka 2024. Uzalishaji wa mpunga umeshuka kwa tani 2,256.8 (kutoka tani 43,658.8 mwaka 2023 hadi tani 41,402.0 mwaka 2024) hii ni kutokana na kuwa eneo kubwa la mpunga la Zanzibar ni la kutegemea mvua na kwa mwaka 2024 uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua umepungua kutoka tani 36,362.4 hadi tani 29,767.5. Aidha, uzalishaji wa mboga na matunda umepungua kwa tofauti ya tani 6,741.6 kutoka tani 87,970.6 mwaka 2023 hadi kufikia tani 80,044.2 mwaka 2024, kutokana na kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya matunda, hasa mapapai na mananasi kwa Pemba.

13. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa zao la biashara la karafuu, uzalishaji umepungua kutoka tani 2,654.6 mwaka 2023 hadi kufikia tani 1,167.4 za mwaka 2024 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 56. Hali hii imetokana na kuwa na msimu mdogo wa uzalishaji pamoja uwepo wa mvua kubwa. Aidha, Wizara inaendelea kuhamasisha wakulima wa zao hili kwa kuwataka kuongeza juhudi katika uzalishaji wenye tija kwa kuwapatia miche bora, elimu ya uoteshaji na uhuishaji.

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mazao ya mifugo, takwimu zinaonesha kuongezeka kwa uchinjaji wa ng'ombe kutoka ng'ombe 29,851 mwaka 2023 hadi ng'ombe 31,953 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 7. Aidha, idadi ya mbuzi na kondoo waliochinjwa imepungua kutoka mbuzi na kondoo 13,977 mwaka 2023 hadi kufikia mbuzi na kondoo 12,084 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 16. (**Kiambatanisho Nam. 2A**). Idadi ya kuku waliochinjwa katika maeneo rasmin imepungua hadi kufikia kuku 1,085,856 mwaka 2024 ukilinganishwa na kuku 1,161,238 mwaka 2023 (**Kiambatanisho Nam. 2B**). Aidha, uchinjaji wa wanyama wengine umeripotiwa kwa ongezeko la bata 3,626 mwaka 2024 kutoka bata 2,865 mwaka 2023, simbilisi 323 na sungura 310 (**Kiambatanisho Nam. 2C**).

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mazao ya misitu, takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2024 matumizi ya kuni yamepungua kutoka mita za ujazo 25,909.7 mwaka 2023 hadi kufikia mita za ujazo 18,764.5 mwaka 2024. Matumizi ya boriti yameongezeka kutoka mita za ujazo 2,053.5 mwaka 2023 hadi mita za ujazo 2,254.5 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 10. Aidha, uzalishaji wa mapau ya kuezekea umepungua kutoka mita za ujazo 2,264 mwaka 2023 hadi kufikia mita za ujazo 1,453.3 mwaka 2024. Uzalishaji wa nguzo kubwa umepungua kutoka mita za ujazo 2,084.8 mwaka 2023 hadi kufikia mita za ujazo 1,259 mwaka 2024 (**Kiambatanisho Nam. 3**). Matumizi ya kuni kwa upande wa wananchi, hasa wa mijini, yamepungua kutokana kuhamasika katika matumizi ya nishati mbadala ya kupikia ikiwemo gesi na umeme. Aidha, kuongezeka kwa gharama za ujenzi kunapelekea jamii kununua malighafi za ujenzi (majengo) kutoka Tanzania bara, vilevile jamii imeongeza wigo wa matumizi mbadala ya vifaa vya ujenzi ikiwemo chuma na *'aluminium'*. Wizara inaendelea kuhamasisha jamii kutumia mbinu mbadala za nishati na ujenzi ili kunusuru misitu na bioanuai zetu.

## MUUNDO NA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO.

16. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imeundwa na Idara sita (6), Taasisi mbili (2) na Ofisi Kuu Pemba; ambazo ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi; Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula; Idara ya Umwagiliaji Maji; Idara ya Misitu na Idara ya Maendeleo ya Mifugo. Kwa upande wa Taasisi ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar (ZALIRI); na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo. Aidha, Wizara ina jumla ya wafanyakazi 2,308 (Unguja 1,749 na Pemba 559) ambao wote ni waajiriwa wa kudumu.

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina majukumu makuu yafuatayo:

    1. Kusimamia maendeleo ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya mifugo, chakula na biashara, huduma za pembejeo na zana za kilimo, miundombinu bora ya

Umwagiliaji, huduma za ugani (elimu kwa wakulima na wafugaji) pamoja na uhifadhi na ukaguzi wa mazao;

2. Kulinda, kuhifadhi na kusimamia rasilimali za misitu na wanyamapori;

3. Kubuni, kupanga na kutekeleza kazi za utafiti wa sekta za kilimo (mazao, mifugo na misitu) na kutoa matokeo yake kwa wadau;

4. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti pamoja na kuratibu mashirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi wakiwemo washirika wa maendeleo na sekta binafsi; na

5. Kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala ikiwa ni pamoja na masuala ya mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu pamoja na uratibu wa masuala mtambuka ikiwemo ukimwi na jinsia.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI 2025

### Mapato Yaliyokusanywa Kulingana na Malengo Yaliyowekwa

18. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo imekadiriwa kukusanya mapato ya TZS bilioni **5.704** kupitia vianzio vyake 11 viliopo Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Wizara imeweza kukusanya TZS bilioni **4.483** sawa na asilimia 99 ya makadirio kwa Julai Machi na asilimia **78.5** ya makadirio ya mwaka (**Kiambatanisho Nam 4).**

### Mafanikio na Changamoto za Utekelezaji

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 Wizara imepata mafanikio yafuatayo:

a. Kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde saba (7) yenye ukubwa wa hekta 1,354; ikiwemo bonde la Kilombero (hekta 292), Cheju A' (hekta 315) na Cheju B' (hekta 301), Kibokwa (hekta 147), Kinyasini (hekta 184), Chaani (hekta 71) na Mlemele (hekta 44). Miundombinu hii imeongeza tija katika uzalishaji wa mpunga kutoka wastani wa tani 3 - 5 kwa hekta hadi kufikia tani 8 - 11 kwa hekta kwa mwaka. Matarajio ni kufikia tani 15 kwa mwaka;

b. Kufuatia kukamilika kwa miundombinu ya umwagiliaji bonde la Cheju B', Serikali imefanikiwa kugawa, kwa awamu ya kwanza, konde 1,011 kwa wakulima wote waliokutikana kabla ya ujenzi ambapo konde takriban 2,335 zimejengwa miundombinu. Konde 1,324 zilizobakia zinatarajiwa kugawiwa katika awamu ya pili itakayohusisha waombaji wapya, ambao tayari wamewasilisha maombi yao,

wakulima waliopisha kilimo cha miwa katika mabonde mengine pamoja na wakulima waliopata changamoto nyengine wakati wa utekelezaji wa miradi ya kilimo na kukosa maeneo ya kuendelea na kilimo;

c. Jumla ya miche 1,209,954 imeoteshwa ikiwemo miche ya misitu 379,302 (326,777 Unguja na Pemba 52,525), mikarafuu 294,693 (73,710 Unguja na 220,983 Pemba), minazi 28,510 (14,788 Unguja na 13,722 Pemba) pamoja na miche ya matunda 507,449 (Unguja 415,529 na 94,940 Pemba);

d. Jumla ya watalii 42,465 walitembelea misitu ya hifadhi wakijumuisha (33,614 nje ya nchi na 8,799 ndani). Aidha, TZS 998,323,034 na Dola za kimarekani 61,075.6 zilikusanywa ikiwa ni ada za viingilio. Vile vile, mradi wa Zipline wenye urefu wa kilomita moja uliochini ya kampuni ya *'Zanzi ecotourism'* tayari umekamilika kwa hatua ya ujenzi njia kuu na unaendelea kwa ujenzi wa miundombinu saidizi ikiwemo Mgahawa;

e. Kwa kushirikiana na Washirika wa ***'OKOA MALIASILI'*** wanaofanyakazi kwa ushirikiano na Taasisi ya ***'Earth Rangers'*** Serikali imepokea msaada wa vifaa vya Mfumo wa Ulinzi wa Maliasili unaoongozwa na Satelite (*Satellite Surveillance System*) kwa lengo la kuongeza uangalizi wa maliasili zetu za misitu, kilimo na wanyamapori ili kudhibiti ujangiri na uvamiziwa maeneo ya Serikali. Mfumo tayari umeshafungwa katika Ofisi za Wizara zilizopo Maruhubi – Misitu na tayari umeanza kazi. Aidha, Mtaalam wa mifumo ya 'Udhibiti wa Uhalifu kwa Wayamapori kwa njia ya Mtandao', Bwana Robert Clement Monday, kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii Tanzania yupo nchini kwa ajili ya kutoa mafunzo na usaidizi kitaalam katika kusimamia mfumo huo. Ili kuimarisha kazi za ulinzi na ufuatiliaji wa maliasili zetu, Serikali inakusudia kuanzisha kitengo cha 'Surveillance' kitakachokuwa chini ya Usimamizi wa Katibu Mkuu kupitia miongozo ya kiutumishi na tunatarajia kuwa na vituo maalum saidizi katika kila Mkoa;

f. Kukamilika kwa 'Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo' unaokusudia kuanzisha vituo vya wakulima katika kila wilaya ambapo elimu na mbinu za kisasa za kilimo zitatolewa ili kuongeza ufanisi katika sekta zote za kilimo. Mpango huo unategemewa kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo kwa kushirikisha Mikoa, Wilaya, mashirika, kampuni binafsi na wadau wa maendeleo katika kuendeleza shughuli za kilimo na mifugo. Lengo kuu la Mpango ni kukibadilisha kilimo cha Zanzibar kutoka kilimo cha kujikimu na kuwa kilimo cha biashara, kinachozingatia taratibu za kilimohai, ambacho kitaweza kwenda sambamba na mahitaji ya masoko ya ndani, yakiwemo ya utalii, na nje ya nchi. Aidha, Wizara imeingia makubaliano ya awali (MoU) na Kampuni ya Uingereza kujenga vituo vya kisasa vya kilimo katika kila wilaya ya Zanzibar, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi;

g. Katika jitihada za kudhibiti magonjwa ya wanyama, kuku 119, 508 (105,722 Unguja na 13,786 Pemba) wamechanjwa dhidi ya magonjwa ya kuku ikiwemo mahepe, gomboro na ndui. Mbwa 5,877 (4,883 Unguja na 994 Pemba) wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na ng'ombe 9,527(836 Unguja na 8,691 Pemba) wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu na kimeta; mapele ya ngozi, ndigana kali na miguu na midomo;

h. Kuimarisha chinjio la Kisakasaka kwa kukarabati sakafu, paa, na kujenga chanja za kuning'inizia minofu baada ya uchinjaji;

i. Kukamilisha ujenzi wa ghala la kuhifadhia chakula liliopo Dodeani lenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 za nafaka sambamba na ukarabati wa maghala mawili (2) ya kuhifadhia chakula yenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,100 yaliyopo Malindi (New ferry 1,300 na Malindi Njiwa wengi 1,800);

j. Kuanzisha TV Kilimo itakayosaidia kuwaunganisha wakulima, wataalamu na wadau wengine wa kilimo kwa lengo la kutoa elimu, taarifa na kusambaza mbinu za kisasa za kilimo ili kuendana na hali ya soko. Katika hili, TV imeshafanikiwa kurusha vipindi 45 vya mahojiano, makala mbali mbali za kilimo 105 na vipindi 7 vya moja kwa moja (mubashara);

k. Kukamilisha majaribio ya aina tisa (9) za mbegu mpya za mpunga katika mabonde sita (6) ya Cheju, Kibonde mzungu na Uzini kwa Unguja, na mabonde ya Kwalempona, Tungamaa na Mlemele kwa Pemba. Lengo ni kuangalia ustahamilivu wa maradhi ya umanjano yanayojuilikana kitaalamu kwa jina la *'Rice Yellow Mottle Virus Diseases - (RYMV)'* na maradhi ya ukungu yanayojulikana kwa jina la *'Rice blast'*. Tathmini imeonesha kwamba aina tatu za mbegu zimefanya vizuri, ambazo ni ZARIC3, ZARIC5 na IR16A-3838;

l. Kufanya utafiti wa aina 10 za mbegu za kienyeji za muhogo ulikuwa na lengo la kuangalia mbegu zenye kuzaa sana, kustahamili maradhi ya michirizi kahawia na batobato. Matokeo ya awali yameonesha kwamba mbegu aina ya machui iliyoimarishwa, ZNZ2018/012, KBH2016B/185, KBH/2018, 1171, 087, 020, REFU na CONTUA 1 zilionesha dalili za ustahamilivu wa maradhi ya michirizi kahawia kwenye majani na shina;

m. Kufanikiwa kuendeleza mradi wa kudhibiti ndege aina ya kunguru kwa awamu ya pili wenye thamani ya jumla ya TZS milioni 300 ambapo hadi sasa jumla ya kunguru 941 wamekamatwa na kushughulikiwa ipasavyo; na

n. Kukamilisha Mkakati wa Kilimo Hai ambao upo kwa Mchapaji Mkuu wa Serikali kwa hatua za mwisho za uchapaji. Aidha, Wizara imetoa, kwa utaratibu maalum,

maghala manne kwa Kampuni ya 'Minjingu Fertilizers' ili kuleta karibu mbolea hai kwa ajili ya kilimo. Vile vile, tumetoa maeneo ya kufanyiakazi kwa Taasisi ya 'Plant Biodefenders' ya Kilimanjaro kwa lengo la kutengeneza na kusambaza pembejeo za Kilimo hai. Kadhalika, Serikali imeanzisha mahusiano na Kampuni ya ***'Tanzania Biotech Products Ltd',*** ya mjini Kibaha, yenye kiwanda kilichopo chini ya Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) inayozalisha viuatifu hai kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa viuatilifu hivyo ambavyo matumizi yake yanatarajiwa kuongeza kinga kwa afya, ardhi na mazingira yetu. Mkataba wa awali unaandaliwa katika kuimarisha mahusiano hayo.

20. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana Wizara hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

    a. Wizara bado inakabiliana na matukio ya uharibifu na wizi wa mazao, ambapo baadhi ya madalali hununua bidhaa za wizi na kuzifikisha sokoni bila kufahamika ambapo inapunguza ari kwa wakulima;

    b. Upungufu wa wataalamu wa kada za kilimo, mifugo na maliasili unaotokana na wimbi kubwa la wataalamu kustaafu au kuhamishiwa sekta nyengine wakiwemo mabibi na mabwana shamba;

    c. Uvamizi wa maeneo ya kilimo unaosababishwa na ongezeko kubwa la ujenzi wa makaazi na shughuli nyengine za kimaendeleo;

    d. Kuendelea kwa athari za mabadiliko ya tabianchi kunakopelekea uhaba wa mvua, maradhi kwa mazao na upungufu wa malisho kwa mifugo;

    e. Kuendelea kwa uharibifu wa misitu unaotokana na shughuli za kibinadamu kama vile uvunaji wa asali kwa kutumia njia za kienyeji; na

    f. Utumiaji holela wa madawa yenye kemikali unaopelekea kuathiri kwa afya ya udongo.

21. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Wizara imechukua hatua zifuatazo:

    a. Kuangalia upya taratibu za udhibiti wa mazao na mifugo mashambani kabla ya kuyasafirisha kuelekea sokoni. Tunaomba vyombo husika viendeleze jitihada za kutatua changamoto ya wizi wa mazao na mifugo;

    b. Kuwasilisha mapendekezo ya uajiri wa kada mbali mbali Ofisi Kuu ya Utumishi Serikalini;

c. Kukamilisha Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo ambapo utekelezaji wake unategemewa kutatua changamoto nyingi za sekta ya kilimo zilizoainishwa;

d. Kuendelea na utaratibu wa kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima kwa bei elekezi na kuzingatia muda sahihi kulingana na msimu husika;

e. Kufanya tafiti juu ya mazao ya kilimo na mifugo yanayohimili athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na kuhamasisha wananchi kulima na kufuga; na

f. Kukamilisha Mpango Mkakati wa Kilimo Hai na Sheria ya Utibabu wa mimea na Ukaguzi wa Mazao ambao utaenda kutatua changamoto ya utumiaji wa madawa yenye kemikali.

**Fedha Iliyopatikana kwa Kipindi cha Utekelezaji**

22. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara iliomba kuidhinishiwa kutumia TZS bilioni **128.107** kupitia Programu zake kuu nne, kati ya fedha hizo TZS bilioni **23.423** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **19.134** kwa Mishahara na TZS bilioni **4.289** kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni **11.197** ikiwa ni Ruzuku (TZS bilioni **9.520** kwa Mishahara na TZS bilioni **1.677** kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

23. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara imeombewa jumla ya TZS bilioni **93.488** (TZS bilioni **63.488** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS bilioni **30.000** kutoka SMZ).

24. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025 Wizara imepata TZS bilioni **27.650** sawa na asilimia 22 ya fedha zilizoidhinishwa, kati ya hizo TZS bilioni **14.675** zimetumika kwa matumizi ya kawaida (TZS bilioni **12.677** kwa mishahara na TZS bilioni **1.998** kwa matumizi mengineyo). Aidha, ruzuku ya Serikali kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta ni TZS bilioni **7.161** (TZS bilioni **6.472** kwa mishahara na TZS milioni **689.372** kwa matumizi mengineyo). Kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Machi, 2025 Wizara imepata TZS bilioni **5.814** (TZS milioni **844.344** kutoka SMZ na TZS bilioni **4.969** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) **(Kiambatanisho Nam. 5).**

**UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 – MACHI 2025.**

25. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesimamia utekelezaji wa malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 - 2026 na Mipango Mikakati ya Kisekta ikiwemo Mpango wa

Maendeleo ya Sekta wa Kilimo. Utekelezaji umesaidia kuongeza uzalishaji na tija hususan kwa mazao ya mboga na matunda.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipanga kutekeleza programu kuu nne na Miradi kumi na mbili (12). ya Maendeleo. Programu hizo ni kama ifuatavyo:

1) Programu ya Maendeleo ya Kilimo;
2) Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
3) Programu ya Maendeleo ya Mifugo; na
4) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

Aidha, Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa ni ifuatayo:

i. Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji;
ii. Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC);
iii. Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula;
iv. Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo;
v. Mradi wa Mageuzi ya uzalishaji wa maziwa kwa wafugaji wadogo unazingatia mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP);
vi. Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR;
vii. Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP);
viii. Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na kuhakikisha usalama wa Chakula (STREPHIT);
ix. Mradi wa KILIMO TIJA;
x. Mradi wa Kudhibiti Sumu kuvu (TANIPAC)
xi. Mradi wa kuwaunganisha wakulima katika masoko kupitia Mnyororo wa Thamani AGRICONNECT; na
xii. Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji (ODA).

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025 Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo ilikusudia kutekeleza shughuli ziuatazo:

a. Kuendelea Kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Wizara;

b. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, maliasili na mifugo ikiwemo ujenzi wa vituo vya huduma za kilimo mawilayani.

c. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ikiwemo ndizi na mpunga, mboga na matunda na uzalishaji wa asali kwa kufanya tafiti, utaalamu na kusambaza teknologia kwa wakulima.

d. Kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi;

e. Kuimarisha upandaji wa miti kwa kuotesha miche 1,700,000 ya Misitu, Mikarafuu, Minazi, Matunda na Viungo na kutathmini hali ya uhuishaji wa miti iliyopandwa;

f. Kuimarisha usimamizi wa misitu pamoja na kuendeleza uwekezaji wa Miradi yenye tija katika hifadhi za misitu;

g. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi; na

h. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi, ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za kisekta.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO**

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu ndogo nne zifuatazo:

i. Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji;
ii. Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula;
iii. Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo; na
iv. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar – ZALIRI.

**Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji maji**

29. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

a. Miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde saba (7) yenye ukubwa wa hekta 1,354; ikiwemo bonde la Kilombero (hekta 292), Cheju A’ (hekta 315) na Cheju B’ (hekta 301), Kibokwa (hekta 147), Kinyasini (hekta 184), Chaani (hekta 71) na Mlemele (hekta 44) yamekamilika kwa asilimia 100. Miundombinu hii imeongeza tija katika uzalishaji wa mpunga kutoka wastani wa tani 3 - 5 kwa hekta hadi tani 8 - 11 kwa hekta kwa mwaka. Matarajio ni kufikia tani 15 kwa mwaka;

b. Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji maji katika bonde la Cheju B’ lenye ukubwa wa hekta 301 limekamilika kwa asilimia 100. Aidha, bonde hilo tayari limeshakabidhiwa kwa serikali ili wananchi waendelee na shughuli zao za kilimo. bonde hilo litawanufaisha zaidi ya wakulima 2,000 wa kilimo cha umwagiliaji maji;

c. Kazi za ujenzi wa kilomita 20 za misingi ya umwagiliaji maji kwa kiwango cha saruji katika mabonde ya Chaani, Kibokwa, Cheju A’, Kilombero na Mlemele zimekamilika; na

d. Ujenzi wa uzio wenye urefu wa mita 300 katika bwawa la Kinyasini umekamilika.

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo hii iliomba kuidhinishiwa TZS bilioni **28.419** kati ya hizo TZS bilioni **2.419** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **1.879** Mishahara na TZS milioni **540.000** kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni **25.500** kwa ajili ya Miradi kutoka washirika wa maendeleo na TZS millioni **500** kutoka SMZ. Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii imepata TZS bilioni **1.499**. Kati ya fedha hizo TZS milioni **1.045** kwa Mishahara, TZS milioni **89.552** kwa matumizi mengineyo na TZS bilioni **364.478** kwa kazi za maendeleo.

**Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.**

31. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

    a. Tathmini ya uzalishaji wa zao la mpunga imefanyika na matokeo ya uzalishaji ni tani 41,409.96 kwa mwaka 2024;

    b. Maghala mawili ya kuhifadhia chakula yaliyopo Malindi (New ferry na Malindi Njiwa wengi) yamekamilika kukarabatiwa kwa lengo la kuhifadhi akiba ya chakula, pamoja na kukamilisha ujenzi wa ghala la Dodeani. Aidha, maghala 9 yanaendelea na ukarabati;

    c. Jumla ya miche 830,652 imezalishwa ikiwemo mikarafuu 294,693 (73,710 Unguja na 220,983 Pemba), minazi 28,510 (14,788 Unguja na 13,722 Pemba) pamoja na miche ya matunda 507,449 (Unguja 415,529 na 94,940 Pemba);

    d. Kampeni za kudhibiti nzi waharibifu wa matunda zimeendelea ambapo jumla ya mitego 12408 ya dawa ya kunasia nzi wa matunda (ME) imepelekwa kwa wakulima na lita 1,161 za dawa ya 'Protein Bait GF 120' imetolewa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali; na

    e. Jumla ya tani 133,575.63 za mazao zimekaguliwa kwa kuingizwa na kusafirishwa nje ya nchi. Kati ya hizo jumla ya tani 120,655.68 zimeingizwa na tani 12,919.95 zimesafirishwa.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo hii iliomba kuidhinishiwa jumla ya TZS bilioni **63.478** kati ya hizo TZS bilioni **5.672** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **4.600** kwa Mishahara na TZS bilioni **1.072** kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu iliombewa TZS bilioni **57.806** kwa miradi ya maendeleo (TZS billion **28.500** kutoka SMZ na TZS bilioni **29.306** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii imepata TZS bilioni **8.026** (TZS bilioni **3.055** ni Mishahara na TZS milioni **279.397** kwa matumizi mengineyo), na kwa fedha za Maendeleo zilizopatikana ni TZS bilioni **4.691** (TZS milioni **330.345** kutoka

SMZ na TZS bilioni **4.361** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 13% ya fedha zilizoombwa.

**Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo**

33. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa Mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

   a. Jumla ya ekari 4,414 zimelimwa (Unguja 2,741.25 na Pemba 1,672.75). WAKALA imefanyia matengenezo madogo madogo matrekta 19 (Unguja 11; Pemba 8). Aidha, ununuzi wa vilainishi na vipuri mbali mbali kwa ajili ya matengenezo ya matrekta umefanyika.

   b. Mikutano na jumuiya za wakulima katika mabonde ya Kilombero na Cheju imefanyika, lengo la mikutano hiyo ni kuhakikisha sekta binafsi zinatoa huduma bora kwa wakulima.

34. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta iliomba kuidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni **2.161** kati ya hizo (TZS bilioni **1.685** Mishahara na TZS milioni **476.100** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii imepata TZS bilioni **1.492** ambapo (TZS bilioni **1.121** kwa ajili ya Mishahara na TZS milioni **371.260** kwa matumizi mengineyo).

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar – ZALIRI**

35. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu ndogo hii kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

   a. Utafiti wa aina 10 za mbegu za kienyeji za muhogo umefanywa Unguja na Pemba ambao ulikuwa na lengo la kuangalia mbegu zenye kuzaa sana, kustahamili maradhi ya michirizi kahawia na batobato. Matokeo ya awali yalionesha mbegu aina machui iliyoboreshwa, ZNZ2018/012, KBH2016B/185, KBH/2018, 1171, 087, 020, REFU na CONTUA 1 zilionesha ukinzani mkubwa dhidi ya dalili za ustahamilivu wa maradhi ya michirizi kahawia kwenye majani na shina;

   b. Pia, jumla ya tafiti 10 za mbegu za viazi lishe (Mdonge, SPZ017/629A, Shangazi Mkubwa, SPZ017/557, SPZ017/1146, SP04, TIJA, SP05, Zambarau na Kizimbani-mayai) ziliendelea. Lengo ni kutathmini vinasaba za viazi vitamu vyenye rangi ya machungwa na zambarau dhidi ya ugonjwa wa ukungu kwenye majani na shina. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa aina ya SP 04, Zambarau, na SPZ017/629A zimeonesha viwango vya juu zaidi vya ustahamilivu wa ugonjwa ya ukungu kwenye kigogo na majani;

c. Aina 9 za mbegu ya mpunga zilifanyiwa majaribio kwenye mabonde sita (6) ya mpunga ambayo ni Cheju, Kibonde mzungu, Uzini, Kwalempona, Tungamaa na Mlemele. Lengo ni kuangalia ustahamilivu wa maradhi ya 'Umanjano' na maradhi ya ukungu. Tathmini imeonesha kwamba aina 3 za ZARIC3, ZARIC5 na IR16A-3838 zilifanya vizuri katika eneo la uzazi mkubwa na kustahamili magonjwa ya umanjano na ukungu;

d. Utafiti wa minyoo kwa mbuzi umefanyika ambapo ukusanyaji wa sampuli za minyoo umeanza kwa Wilaya ya Kusini, Kaskazini B', Kati, Magharibi A', Chakechake, Wete, Mkoani na Micheweni. Aidha, utafiti huu umejumuisha wafugaji wa nane (8) kwa kila Shehia ambapo wastani wa mbuzi 3 – 5 wamechukuliwa sampuli za minyoo na unatarajiwa kuendelea katika msimu wa mvua za masika za mwaka 2025.

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar iliomba kuidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni **9.035**, kati ya hizo (TZS bilioni **7.835** Mishahara na TZS bilioni **1.200** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii imepata TZS bilioni **5.669** (TZS bilioni **5.351** kwa Mishahara na TZS milioni **318.112** kwa matumizi mengineyo).

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU**

37. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hii ndogo kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

a. Jumla ya watalii 42,465 walitembelea misitu ya hifadhi wakijumuisha (33,614 nje ya nchi na 8,799 ndani). Aidha, TZS 998,323,034 na Dola za kimarekani 61,075.6 zilikusanywa ikiwa ada za viingilio. Mradi wa Zipline uliochini ya kampuni ya Zanzi ecotourism umekamilika kwa hatua ya ujenzi wa njia kuu ya waya;

b. Jumla ya miche 379,302 imeoteshwa kupitia vitalu vya Serikali. Miongoni mwa miche hiyo, miche 326,777 imeoteshwa Unguja na miche 52,525 imeoteshwa Pemba;

c. Jumla ya hekta 40.31 zimepandwa miti. Kati ya hizo, hekta 31.31 zimepandwa mikoko (9.81 Unguja na 21.5 Pemba) na hekta 9 zimepandwa miti ya misitu katika hifadhi za Serikali ikiwemo hekta 5 hifadhi ya Chaani-Masingini na hekta 4 hifadhi ya Dunga;

d. Andiko la awali la mradi wa kupandisha hadhi msitu wa Mtambwe limekamilika na limewasilishwa kwa mfadhili ambae ameonesha nia ya kulikubali. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2025/2026;

e. Jumla ya doria 390 (247 Unguja na 143 Pemba) zimefanyika katika maeneo ya rasimali za misitu ambapo matukio 134 (64 Unguja na 70 Pemba) yanayohusu uharibifu na ukataji wa misitu, usafirishaji wa mazao ya misitu bila ruhusa, uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa kilimo na ujenzi wa nyumba za makaazi, ukataji wa miti ndani ya hifadhi na matumizi mabaya ya misumeno ya moto, yameripotiwa;

f. Uzalishaji wa asali unaendelea kuhamasishwa ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya tani 7.27 (4.98 Pemba na 2.29 Unguja) zimezalishwa; na

g. Utafiti wa ndege unaolenga kutambua mwenendo, idadi, uzito na mayai unaofadhiliwa na mradi wa 'Heshimu Bahari' kwa kushirikiana na Idara ya Uvuvi, na Shirika la uhifadhi Wanyamapori na mimea Duniani (WCS) umeanza kwa ukusanyaji wa taarifa za awali. Utafiti huo unafanyika katika eneo lote la Fungu Mbaraka.

38. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu iliomba kuidhinishiwa TZS bilioni **3.418** kati ya hizo (TZS bilioni **2.888** Mishahara, TZS millioni **530.00** kwa matumizi mengineyo na TZS bilioni **1.183** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii imepata TZS bilioni **2.933** ambapo TZS bilioni **1.846** kwa mishahara, TZS milioni **479.213** kwa matumizi mengineyo na TZS milion **608.118** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

39. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina Programu ndogo mbili za Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo.

### Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo

40. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hizi ndogo kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

a. Ng'ombe 1,729 (1, 152 Unguja na 577 Pemba) wamepandishwa kwa njia ya sindano;

b. Ekari saba (7) ya malisho aina ya **JUNCAO** yamepandwa kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu za malisho na kuwapatia wafugaji 121 (106 Unguja na 15 Pemba);

c. Mafunzo 6 (4 Unguja na 2 Pemba) yametolewa kwa wafugaji 143 wa kuku na 92 wa ng'ombe wa maziwa ili kujua mbinu bora za ufugaji wa ng'ombe na kuku kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao ya mifugo Unguja na Pemba;

d. Wafugaji 11,323 (4,841 Unguja na 6,482 Pemba) wametembelewa na kupewa ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye kuleta tija kwa wafugaji;

e. Katika jitihada za kudhibiti magonjwa ya wanyama, kuku 119, 508 (105,722 Unguja na 13,786 Pemba) wamechanjwa dhidi ya magonjwa ya kuku ikiwemo mahepe, gomboro na ndui. Mbwa 5,877 (4,883 Unguja na 994 Pemba) wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na ng'ombe 9,527 (836 Unguja na 8,691 Pemba) wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu na kimeta, mapele ya ngozi, ndigana kali na miguu na midomo;

f. Wanyama 152 (mbwa 43 na paka 109) wamefungwa kizazi ili kupunguza idadi ya mbwa na paka wazururaji;

g. Sampuli 1,834 (986 Unguja na 848 Pemba) zilichunguzwa maradhi mbalimbali katika maabara, sampuli 617 ndizo zilizoonekana na vimelea vya maradhi ya kuharisha damu na minyoo kwa kuku, kwa mbwa kichaa cha mbwa, kwa ng'ombe ndigana kali, ugonjwa wa kiwele na minyoo na kwa upande mbuzi minyoo na usugu wa vimelea vya maradhi dhidi ya madawa. Sampuli hizo zimechunguzwa kwenye kinyesi, ubongo, damu na maziwa.

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo iliomba kuidhinishiwa TZS bilioni **13.245** kwa matumizi ya kawaida na maendeleo (TZS bilioni **3.085** kwa Mishahara na TZS millioni **660.500** kwa matumizi mengineyo). Aidha, iliombewa TZS bilioni **9.500** kwa miradi ya maendeleo (TZS bilioni **2.00** kutoka SMZ na TZS bilioni **7.500** kutoka kwa washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni **2.459**, ambapo TZS bilioni **2.209** kwa mishahara na TZS milioni **99.734** kwa matumizi mengineyo na TZS milioni **149.521** kutoka SMZ kwa ajili ya maendeleo.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu ndogo tatu ambazo ni:

i. Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo;
ii. Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo; na
iii. Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za WKUMM - Pemba.

### Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo

43. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu Ndogo hii kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

a. Wafanyakazi 620 wamepatiwa stahiki zao ikiwemo ubani (95) likizo (324) na muda wa ziada (201) ambapo jumla ya TZS 98,594,356.30 zimetumika;

b. Jumla ya wafanyakazi kumi na tisa (167) walipatiwa mafunzo ya muda mrefu (158) na muda mfupi (9) ambapo jumla ya TZS 71,828,000 zimetumika; na

c. Wizara imewasilisha orodha ya maeneo ya ardhi yanayohitaji kusajiliwa kwa Wizara ya Ardhi.

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji iliomba kuidhinishiwa TZS bilioni **2.829** kwa kazi za kawaida (TZS bilioni **2.080** kwa Mishahara na TZS millioni **749.000** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu Ndogo hii imepata TZS bilioni **1.893** (TZS bilioni **1.268** kwa mishahara na TZS milioni **625.108** kwa matumizi mengineyo).

**Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo**

45. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu ndogo hii kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo;

a. Kukamilika kwa Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo unaokusudia kuanzisha vituo vya wakulima kila wilaya ambapo elimu na mbinu za kisasa za kilimo zitatekelezwa ili kuongeza ufanisi katika sekta zote za kilimo;

b. Sheria mpya ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo ipo katika hatua ya kuwasilishwa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya maamuzi. Sheria na Sera ya Kilimo na Sheria na Sera ya Misitu zipo katika hatua ya kupelekwa katika kikao cha makatibu wa Kuu;

c. Waraka wa machinjio tayari umepatiwa maamuzi na Serikali ambapo jukumu la kufanya ukaguzi wa mnyama kabla na baada ya kuchinjwa limerejeshwa Wizara yenye dhamana ya mifugo kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Mifugo Namba 11 ya mwaka 1999; na

d. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeshiriki Utafiti wa Kitaifa wa Sampuli za Kilimo (National Agricultural Sample Survey) kwa lengo la kujua hali halisi ya kilimo.

46. **Mheshimiwa Spika** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii ndogo iliomba kuidhinishiwa TZS milioni **826.598** kwa kazi za kawaida (TZS milioni **490.498** Mishahara na TZS milioni **336.100** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii Ndogo imepata TZS milioni **351.194** (TZS milioni **268.116** kwa mishahara na TZS milioni **83.078** kwa matumizi mengineyo).

**Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba**

47. **Mheshimiwa Spika,** shabaha zilizotekelezwa na Programu hii ndogo kwa mwaka 2024/2025 ni kama ifuatavyo:

a. Kuratibu vikao na ziara za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kisiwani Pemba;

b. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, vituoni na mashambani;

c. Kuratibu ziara za wageni na viongozi pamoja na kuhudhuria katika vikao, sherehe na kumbukumbu za kitaifa; na

d. Kutatua changamoto za wadau pamoja na kuimarisha mashirikiano na taasisi nyengine (za Serikali, Sekta binafsi, na Taasisi za Kijamii).

48. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu hii ndogo iliomba kuidhinishiwa TZS bilioni **4.513** kwa kazi za kawaida (TZS bilioni **4.112** Mishahara na TZS millioni **401.000** kwa matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi, 2025 Programu hii ndogo imepata TZS bilioni **3.327** (TZS bilioni **2.985** kwa mishahara na TZS milioni **341.855** kwa matumizi mengineyo).

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### Makadirio ya Mapato

49. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imekadiriwa kukusanya mapato ya TZS bilioni **8.241** kupitia vianzio vyake viliopo Unguja na Pemba **(Kiambatanisho Nam. 6A).**

### Makadirio ya Matumizi 2025/2026

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, inaomba kuidhinishiwa kutumia **TZS bilioni 92.728** kupitia Programu zake kuu nne, kati ya fedha hizo TZS bilioni **23.270** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **18.018** kwa Mishahara na TZS bilioni **5.252** kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni **11.276** ikiwa ni Ruzuku (TZS bilioni **8.531** kwa Mishahara na TZS bilioni **2.745** kwa matumizi mengineyo) kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo, na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo (**Kiambatanisho Nam. 6B).**

51. **Mheshimiwa Spika,** kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara inaombewa jumla ya TZS bilioni **58.183** (TZS bilioni **33.483** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS bilioni **24.700** kutoka SMZ) (**Kiambatanisho Nam. 6B).**

## MALENGO YA PROGRAM ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Wizara ya Kilimo Uwagiliaji Maliasili na Mifugo itatekeleza Malengo yafuatayo:

1. Kuendelea Kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ya Wizara;

2. Kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, maliasili na mifugo ikiwemo ujenzi wa vituo viwili vya kutolea huduma kimoja Unguja na Kimoja Pemba;

3. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ikiwemo ndizi na mpunga, mboga na matunda, asali na uzalishaji wa mazao ya mifugo kwa kufanya tafiti, utaalamu na usambazaji teknologia kwa wakulima;

4. Kuendeleza utoaji wa huduma za ukulima na zana za kilimo kwa wakulima pamoja na ushajiishaji wa sekta binafsi;

5. Kuimarisha upandaji wa miti kwa kuotesha miche 1,700,000 ya Misitu, Mikarafuu, Minazi, Matunda na Viungo na kutathmini hali ya uhuishaji wa miti iliyopandwa;

6. Kuimarisha usimamizi wa misitu pamoja na kuendeleza uwekezaji wa Miradi yenye tija katika hifadhi za misitu;

7. Kutoa maslahi kwa wafanyakazi na kuweka mazingira bora ya kazi; na

8. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi, ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za kisekta.

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA KILIMO**

**Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji**

53. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu Ndogo ya Maendeleo ya Umwagiliaji itatekeleza shabaha zifuatazo:

1. Kufanya mapitio ya 'Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji wa mwaka 2002' (Irrigation Master Plan);

2. Kufanya ukarabati wa mabonde 10 ya umwagiliaji maji ya Mtwango, Mwera, Bumbwisudi, Kibokwa, Kianga, Saninga, Kinyakuzi, Weni, Makombeni na Tibirinzi;

3. Kufanya ukarabati wa visima na mampu katika mabonde ya umwagiliaji maji; na

4. Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji kwa njia ya matone (drip irrigation).

54. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo hii inaombewa kuidhinishiwa TZS bilioni **24.371** kati ya hizo TZS bilioni **2.116** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **1.549** Mishahara na TZS milioni **567** kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni **22.056** kwa ajili ya Miradi kutoka washirika wa maendeleo na TZS millioni **200.000** kutoka SMZ.

**Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika Chakula**

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo ya Kilimo na Uhakika Chakula itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

    1. Kuzalisha miche 700,000 (200,000 ya minazi, 500,000 ya mikarafuu);
    2. Kuimarisha utoaji wa elimu kwa wakulima;
    3. Kufanya ukarabati na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia akiba ya chakula;
    4. Kufanya tathmini ya uzalishaji wa mpunga;
    5. Kusimamia uzalishaji wa mbegu bora za nafaka;
    6. Kudhibiti miripuko ya wadudu na maradhi ya mimea.

56. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Kilimo na Uhakika wa Chakula inaomba kuidhinishiwa jumla ya TZS bilioni **29.908** kati ya hizo TZS bilioni **5.152** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **4.401** kwa Mishahara na TZS milioni **750.846** kwa matumizi mengineyo). Aidha, programu inaombewa TZS bilioni **24.756** kwa miradi ya maendeleo (TZS billion **20.000** kutoka SMZ na TZS bilioni **4.756** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar (ZALIRI).**

57. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo hii inajumuisha shughuli za Utafiti wa Kilimo na Mifugo na itatekeleza shabaha zifuatazo:

    1. Kuendelea na tafiti 10 (4 za kilimo na maliasili; pamoja na tafiti 6 za mifugo) ikiwemo:
        - Matumizi ya karafuu na kungumanga kwa ajili ya kupambana na wadudu waharibifu;
        - Athari za mutajenesi iliyosababishwa na Ethyl Methanosulphanet EMS kwa mavuno ya tungule;
        - Utafiti wa miti adimu iliyohatarini kutoweka;
        - Utafiti wa maziwa kwa wafugaji;
        - Tafiti ya minyoo ya mbuzi; na
        - Utafiti wa matumizi ya mwani kwa ajili ya chakula cha kuku.

2. Kuimarisha miundombinu ya utafiti ikiwemo kujenga na kukarabati baadhi ya majengo;

3. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi kwa kufanya mafunzo ya muda mrefu au mfupi; na

4. Kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi ikiwemo ununuzi wa vifaa na huduma za kiofisi.

58. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar inaomba kuidhinishiwa ruzuku ya TZS bilioni **8.354**, kati ya hizo (TZS bilioni **6.913** Mishahara na TZS bilioni **1.440** kwa matumizi mengineyo).

**Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo**

59. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo itatekeleza shabaha zake kama zifuatazo:

1. Kuendeleza utoaji wa huduma za Matrekta na zana za Kilimo za Serikali, pamoja na kuhakikisha kuwepo vifaa vya kazi, vipuri na vilainishi; na

2. Kuhamasisha sekta binafsi katika kuekeza utoaji wa huduma za Matrekta na zana za kilimo.

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta inaomba kuidhinishiwa ruzuku ya jumla ya TZS bilioni **2.922** kati ya hizo (TZS bilioni **1.617** Mishahara na TZS bilioni **1.305** kwa matumizi mengineyo).

**PROGRAMU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU**

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

i. Kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje ya nchi wanaotembelea hifadhi kutoka 64,000 hadi kufikia 100,000 kwa kuimarisha vivutio na kuhamasisha miradi ya uwekezaji katika maeneo ya hifadhi za Misitu kwa lengo la kuongeza mapato;

ii. Kukamilisha taratibu za upandishaji hadhi Msitu wa Mtambwe na kukamilisha utafiti ya miradi ya kuinua kipato cha wanajamii wanaoishi karibu na misitu hiyo;

iii. Kuotesha miche 1,000,000 (800,000 Misitu na 200,000 Matunda na Viungo) na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahudumu 165;

iv. Kuhamasisha na kupanda miti hekta 130 (hekta 100 misitu ya Serikali, na hekta 30 maeneo ya mikoko) pamoja na kufanya tathmini ya hali ya ukuaji;

v. Kuendeleza na kutoa elimu kwa jamii na kuimarisha ulinzi kwa kufanya doria 500 katika maeneo ya misitu ya hifadhi na misitu ya jamii kwa lengo la kupunguza matukio ya uharibifu;

vi. Kuanzisha kituo cha mafunzo ya Nyuki yatakayojumuisha mafunzo ya Ufugaji, Usimamizi na Ujasiriamali kwa Mazao ya nyuki;

vii. Kuengeza uzalishaji wa asali na mazao mengine ya nyuki kutoka tani 13 kufikia tani 17 kwa kutoa elimu bora ya ufugaji, utunzaji wa kumbukumbu na kuhamasisha kwa ugawaji wa vifaa vya kufugia nyuki; na

viii. Kufanya tafiti ya kubaini idadi aina na hali ya wanyamapori kwa lengo la kuandaa mpango wa kunusuru wanyama waliohatarini kutoweka pamoja na kusimamia mazizi.

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni **7.460** kati ya hizo TZS bilioni **4.040** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **2.606** Mishahara na TZS bilioni **1.434** kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni **3.420** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (TZS bilioni **1.420** kutoka washirika wa maendeleo na TZS bilioni **2.000** kutoka SMZ).

## PROGRAMU YA MAENDELEO YA MIFUGO

### Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

1. Kupandisha ng’ombe 2,000 (1,200 Unguja na 800 Pemba) kwa njia ya sindano;
2. Kupanda eka 10 za malisho katika shamba la malisho Kizimbani kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu za majani ya malisho ya mifugo na kuanzisha mashamba darasa ya malisho kwa kila Wilaya;
3. Kutoa mafunzo 20 (12 Unguja na 8 Pemba) ya mbinu bora za ufugaji wa ng’ombe, mbuzi na kuku kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa mazao;
4. Kuwatembelea wafugaji 17,000 (Unguja 9,000 na Pemba 8,000) na kuwapa ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye kuleta tija kwa wafugaji;
5. Kuanzisha mashamba darasa ya kuku na sungura kwa wafugaji wanawake na vijana kila Wilaya;
6. Kuchanja kuku 250,000 (180,000 Unguja na 70,000 Pemba) dhidi ya ugonjwa wa mahepe, gumboro na ndui, mbwa 8,000 (Unguja 5,000 na Pemba 3,000) dhidi ya

ugonjwa wa kichaa cha mbwa na ng'ombe 35,000 (23,000 Unguja na 12,000) dhidi ya magonjwa chambavu, kimeta, ugonjwa wa mapele ya ngozi na ugonjwa wa miguu na midomo; na

7. Kuchunguza sampuli 1,500 (1,000 Unguja na 500 Pemba) za maradhi ya mifugo.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni **11.463** kati ya hizo TZS bilioni **3.713** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (TZS bilioni **3.016** Mishahara na TZS milioni **697.067** kwa matumizi mengineyo). Aidha, TZS bilioni **7.750** kwa ajili ya Miradi ya maendeleo (TZS bilioni **5.250** kutoka washirika wa maendeleo na TZS bilioni **2.500** kutoka SMZ).

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO

### Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

i. Kuendelea na utoaji wa maslahi ya wafanyakazi 65, ikiwemo ubani (20), likizo (30), na muda wa ziada (15);

ii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 22 kwa masomo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi pamoja na wanafunzi (madaktari wa mifugo 25);

iii. Kuwapatia mafunzo ya kujiandaa na kustaafu wafanyakazi 50;

iv. Kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali TZS bilioni 8.241; na

v. Kusimamia na kudhibiti mali za Serikali kwa kusimamia upimaji wa mashamba matano (5).

66. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni **2.909** kwa kazi za kawaida (TZS bilioni **1.859** kwa Mishahara na TZS bilioni **1.050** kwa matumizi mengineyo).

### Mipango, Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo

67. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti itatekeleza shabaha zake kama ifuatavyo:

i. Kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango, sera na miradi iliyopo chini ya Wizara;

ii. Kuimarisha ukusanyaji wa Takwimu za kisekta;

iii. Kuendeleza mashirikiano na Taasisi za ndani, Kikanda na Kimataifa; na

iv. Kufanya tafiti mbili za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Ajenda ya utafiti wa Zanzibar.

68. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti inaomba kuidhinishiwa TZS milioni **739.426** kwa kazi za kawaida (TZS milioni **384.426** Mishahara na TZS milioni **355** kwa matumizi mengineyo).

**Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo – Pemba**

69. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa shughuli za Kilimo Umwagiaji Maliasili na Mifugo - Pemba itatekeleza shabaha yake kuu ambayo ni Kuratibu na kusimamia kazi za kilimo umwagiliaji maliasili na mifugo Pemba

70. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za kilimo umwagiliaji maliasili na mifugo Pemba inaomba kuidhinishiwa TZS bilioni **4.601** kwa kazi za kawaida (TZS bilioni **4.202** Mishahara na TZS millioni **398.386** kwa matumizi mengineyo).

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

71. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, inakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya TZS bilioni **8.241** kupitia vyanzo vyake Unguja na Pemba.

72. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, inaomba kuidhinishiwa kutumia TZS bilioni **92.728,** kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo zikijumuisha ruzuku ya TZS bilioni **11.276** kwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo pamoja na Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza miradi Kumi na tatu (13) kama inavyoonekana kwenye **Kiambatanisho Nam. 7A – 7L.** Utekelezaji wa Miradi hiyo inaombewa TZS bilioni **58.183** (TZS bilioni **24.700** kutoka SMZ na TZS bilioni **33.482** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Aidha, Wizara itatelekeza Programu Kuu nne kama zinavyoonekana katika **Kiambatanisho Nam 8.**

**SHUKURANI**

74. **Mheshimiwa Spika,** baada ya uwasilishaji huo, sasa natumia nafasi hii kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi za ndani kwa kuendeleza mashirikiano katika kutoa huduma za kilimo, maliasili na mifugo; zikiwemo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais; Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ; Ofisi ya Rais - Kazi Uchumi na

Uwekezaji; Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi; Wizara ya Afya (ZFDA); Wizara ya Maji, Nishati na Madini; Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano; Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale; na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

75. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani za pekee ziende kwenye Wizara na Taasisi zinazoshabihiana na Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kwa upande wa Tanzania Bara. Wizara na Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wakala wa Mbegu Tanzania (ASA), CARI, NFRA, Uongozi wa Mikoa ya Morogoro, Tanga, Arusha na Kilimanjaro.

76. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuyashukuru Mashirika binafsi ya ndani na nje ya nchi yakiwemo PBZ, CRDB, EQUITY BANK, ADB, ZSTC, PDF, TAHA, Plant Biodefenders, UWAMWIMA, FEED THE FUTURE, COSTECH, COMMUNITY FOREST PEMBA, Milele Zanzibar Foundation, ENABEL, TAFIRI, Taasisis ya PPIZ, TALIRI, TPHPA, Kampuni ya Utengenezaji wa mbolea ya Minjingu, TPRI, ZAASO na ZSPCA. Tunazishukuru pia nchi na Mashirika ya Kimataifa yaliyoisaidia kuendeleza sekta hii, zikiwemo Japan, China, Korea ya Kusini, Marekani, UAE, Oman, Italy na Uholanzi, kwa kushirikiana na sisi kuendeleza sekta ya Kilimo. Benki ya Dunia, Benki ya Tanzania ya Kilimo, Benki ya Umoja wa nchi za Ulaya - EU, Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), WFP, ICRAF, IFAD, UNDP, JICA, USAID, USDA, KOICA, IITA, IRRI, WCS, GARC, PASS, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Root and Shoot, Solidaridad, NMB, Heifer International, Exim Bank ya Korea, FLI ya Ujerumani na World Vegetable Centre.

77. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru viongozi wa Wizara hii ninayoiongoza wakiwemo; Katibu Mkuu – Ndugu Ali Khamis Juma, Naibu Katibu Mkuu – Dk. Omar Ali Amir, Afisa Mdhamini WKUMM, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Wizara na Bodi ya Ushauri Jozani pamoja na watumishi wote kwa juhudi zao, ushirikiano na ushauri walionipatia jambo ambalo limeniwezesha kusimama hapa leo hii kuwasilisha Hotuba ya Bajeti kwa mwaka huu.

Pia, nawapongeza kwa dhati viongozi wa Jumuiya za Wakulima na Wafugaji, Wakulima, Wafugaji, Watunza mazingira na Wadau wote wa Sekta za Kilimo, Maliasili na Mifugo kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo kwa ajili ya chakula na biashara pamoja na utunzaji wa misitu nchini.

78. **Mheshimiwa Spika,** Napenda kuwashukuru Viongozi Wateule wote wa Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri, Masheha, Vikosi vya SMZ na SMT na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri wanayoendelea kuyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu.

Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa Hotuba hii ya Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, kwa wakati.

79. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho Waheshimiwa Wajumbe **nakushukuruni kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja.**




**MHE. SHAMATA SHAAME KHAMIS**
**WAZIRI,**
**WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO, ZANZIBAR**

## VIAMBATANISHO


**Kiambatanisho Nam. 1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga, 2023 -2024, Zanzibar**

| Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Mboga 2023 - 2024 - Zanzibar | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **ZAO** | **2023** | | **2024** | |
| | **Eneo lillilopndwa (ekari)** | **Uzalishaji (tani)** | **Eneo lillilopndwa (ekari)** | **Uzalishaji (tani)** |
| Muhogo | 37,548.9 | 220,411.8 | 20,080.4 | 117,871.7 |
| Mpunga wa juu | 25,591.3 | 36,362.4 | 24,565.4 | 29,767.5 |
| Mpunga wa Kumwagilia | 3,928.2 | 7,296.5 | 5,749.8 | 11,634.5 |
| Migomba | 8,664.4 | 74,514.1 | 7,303.3 | 62,808.3 |
| V/vikuu | 1,848.3 | 9,241.3 | 2,876.7 | 14,293.4 |
| Majimbi | 1,192.3 | 4,554.0 | 2,031.1 | 7,758.6 |
| J/kunde | 2,558.9 | 1,279.4 | 2,702.7 | 1,351.4 |
| V/Vidogo | 7,702.1 | 53,914.4 | 6,655.2 | 46,586.6 |
| Mtama | 744.0 | 282.7 | 860.2 | 326.9 |
| N/nyasa | 1,454.3 | 698.0 | 1,082.1 | 519.4 |
| Mahindi | 6,294.2 | 3,147.1 | 4,009.2 | 2,004.6 |
| Mbaazi | 850.8 | 2,748.3 | 847.9 | 2,738.8 |
| Uwele | 386.3 | 77.3 | 323.1 | 64.6 |
| Maboga | 1,420.0 | 6,730.9 | 954.5 | 4,524.2 |
| Chooko | 950.8 | 380.3 | 1,361.4 | 544.6 |
| Mboga na matunda | 21,379.8 | 87970.6 | 23,265.0 | 80,044.2 |
| **Jumla** | **122,514.2** | **527,800.0** | **104,667.8** | **382,929.2** |


**Kiambatanisho Nam. 2A: Idadi ya Mifugo iliyokaguliwa na Kuchinjwa, 2024**




**Kiambatanisho Nam. 2B: Idadi ya Kuku waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2024**



**Kiambatanisho Nam. 2C: Idadi ya Wanyama Wengine waliokaguliwa na Kuchinjwa, 2024.**



**Kiambatanisho Nam. 3: Uzalishaji wa Mazao ya Misitu kwa Mwaka 2024.**



**Kiambatanisho Nam. 4: Ukusanyaji wa Mapato, Julai 2024 - Machi 2025**

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2024/2025 | MAKADIRIO (JULAI - MACHI) | MAKUSANYO (JULAI-MACHI) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | | | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 51,567,000 | 38,850,000 | 42,593,880 | 110 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 2,000,000 | 150,000 | 1,781,000 | 1187 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 100,000,000 | 100,000,000 | - | 0 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 32,000,000 | 23,030,000 | 24,082,501 | 105 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 18,000,000 | 12,450,000 | 20,842,460 | 167 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 2,000,000 | 1,485,000 | 1,820,000 | 123 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI | 15,000,000 | 12,900,000 | 8,415,500 | 65 |
| 1422126 | ADA YA MAZAO YA KILIMO | 500,000 | 460,000 | - | 0 |
| 1422068 | ADA YA MAZAO YA MIFUGO | 550,000 | 250,000 | - | 0 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 35,000,000 | 34,500,000 | 54,991,500 | 159 |
| | **JUMLA PEMBA** | **256,617,000** | **224,075,000** | **154,526,841** | **69** |
| **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA** | | | | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 320,000,000 | 243,100,000 | 337,955,044 | 139 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 26,000,000 | 6,800,000 | 1,500,500 | 22 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI | 1,400,000,000 | 1,124,500,000 | 1,167,337,042 | 104 |
| | **JUMLA** | **1,746,000,000** | **1,374,400,000** | **1,506,792,586** | **110** |
| **IDARA YA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA** | | | | | |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 177,000,000 | 142,600,000 | 168,504,651 | 118 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 15,000,000 | - | - | 0 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 10,000,000 | 7,000,000 | 2,951,500 | 42 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 70,000,000 | 68,000,000 | 112,077,700 | 165 |
| | **JUMLA** | **272,000,000** | **217,600,000** | **283,533,851** | **130** |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | | | | | |
| 1423002 | MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE | 15,000,000 | 13,200,000 | 2,015,000 | 15 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 30,000,000 | - | - | 0 |
| 1422066 | ADA YA UINGIZAJI WAGENI | 30,000,000 | 45,000,000 | 21,016,800 | 47 |
| | **JUMLA** | **75,000,000** | **58,200,000** | **23,031,800** | **40** |
| **IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO** | | | | | |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 2,757,450,000 | 2,084,326,000 | 2,255,443,319 | 108 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 45,000,000 | 33,750,000 | 3,075,000 | 9 |
| | **JUMLA** | **2,802,450,000** | **2,118,076,000** | **2,258,518,319** | **107** |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA** | | | | | |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | 551,433,000 | **516,433,000** | **256,608,000** | 50 |
| | **JUMLA** | **551,433,000** | **516,433,000** | **256,608,000** | 50 |
| | **JUMLA UNGUJA** | **5,446,883,000** | **4,284,709,000** | **4,328,484,556** | **101** |
| | **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | **5,703,500,000** | **4,508,784,000** | **4,483,011,397** | **99** |

**Kiambatanisho Nam. 5: Uchambuzi wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi kwa Kipindi cha Julai 2024 Hadi Machi, 2025.**

| PROGRAM KUU/ PROGRAM NDOGO | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 - MACHI, 2025 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MSHAHARA | MATUMIZI KAWAIDA | RUZUKU MSHAHARA | RUZUKU KAWAIDA | MAENDELEO SMZ | MAENDELEO MUHISANI | JUMLA |
| **PL0101: Maendeleo ya Kilimo** | | | | | | | **13,937,304,554** |
| SL010101: Kuendeleza miundombinu ya Umwagiliaji maji | 1,045,564,818 | 89,552,000 | 0 | 0 | 364,477,843 | 0 | 1,499,594,661 |
| SL010102: Utafiti na Mafunzo ya kilimo - ZARI | 0 | 0 | 2,814,304,874 | 104,768,475 | 0 | 0 | 2,919,073,349 |
| SL010103: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 3,055,428,444 | 279,397,100 | | | 330,345,539 | 4,361,204,950 | 8,026,376,033 |
| SL010105: Karakana ya Matrekta | 0 | 0 | 1,121,000,511 | 371,260,000 | 0 | 0 | 1,492,260,511 |
| **PL0102: Maendeleo ya Raisilimali za Misitu** | | | | | | | **2,933,119,731** |
| SL010201: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 1,845,788,945 | 479,212,786 | 0 | 0 | 0 | 608,118,000 | 2,933,119,731 |
| **PL0103: Maendeleo ya Mifugo** | | | | | | | **4,471,035,397** |
| SL010301 Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 2,209,469,002 | 99,734,000 | 0 | 0 | 149,520,620 | 0 | 2,458,723,622 |
| SL010303: Taasisi ya Utafiti wa Mifugo - ZALIRI | 0 | 0 | 1,876,203,250 | 136,108,525 | 0 | 0 | 2,012,311,775 |
| **PL0105: Mipango na Usimamizi wa Kilimo Maliasili na Mifugo** | | | | | | | **6,308,679,366** |
| SL010501: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 1,267,612,247 | 625,108,349 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1,892,720,596 |
| SL010502: Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 268,116,228 | 83,078,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 351,194,228 |
| SL010503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo - Pemba | 2,985,303,439.50 | 341,854,613 | 660,371,489.50 | 77,235,000 | 0 | 0 | 4,064,764,542 |
| **JUMLA KUU** | **12,677,283,123.50** | **1,997,936,848.00** | **6,471,880,124.50** | **689,372,000** | **844,344,002** | **4,969,322,950** | **27,650,139,048** |

**Kiambatanisho Nam. 6A: Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026**

| KASMA NAMBA | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2025/2026 |
|---|---|---|
| **OFISI KUU PEMBA** | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 74,514,700 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 2,890,000 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 144,500,700 |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 46,240,300 |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 26,010,200 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 2,890,000 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI NGEZI | 21,675,200 |
| 1422126 | ADA YA MAZAO YA KILIMO | 722,500 |
| 1422068 | ADAYA MAZAO YA MIFUGO | 794,700 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 50,575,200 |
| | **JUMLA PEMBA** | **370,813,500** |
| **IDARA YA MISITU** | | |
| 1422022 | ADA YA MAZAO YA MISITU | 463,973,000 |
| 1421001 | MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 26,000,000 |
| 1422066 | UINGIZAJI WA WAGENI JOZANI | 2,033,010,000 |
| | **JUMLA** | **2,522,983,000** |
| **IDARA YA KILIMO NA UHAKIKA WA CHAKULA** | | |
| 1422048 | ADA UKAGUZI WA MAZAO | 255,766,554 |
| 1422060 | MAPATO YA MASHAMBA | 21,675,100 |
| 1421001 | MAUZO YA MICHE | 14,450,000 |
| 1422127 | MAUZO YA PEMBEJEO | 101,150,500 |
| | **JUMLA** | **393,042,154** |
| **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | | |
| 1423002 | MAUZO YA TEKNOLOJIA ZA KILIMO | 21,675,100 |
| 1422066 | ADA YA UINGIZAJI WAGENI | 86,700,500 |
| | **JUMLA** | **108,375,600** |
| **IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO** | | |
| 1421011 | UTIBABU WA WANYAMA | 4,034,535,800 |
| 1422068 | MAPATO YA MIFUGO | 15,025,300 |
| | **JUMLA** | **4,049,561,100** |
| **WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO** | | |
| 1421014 | HUDUMA ZA MATREKTA | 796,824,801 |
| | **JUMLA** | **796,824,801** |
| | **JUMLA UNGUJA** | **7,870,786,655** |
| | **JUMLA KUU UNGUJA NA PEMBA** | **8,241,600,155** |

**Kiambatanisho Nam. 6B: Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/2026.**

| MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA PROGRAMU KUU KWA MWAKA 2025/2026, | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Program | Makadirio | Mshahara | Matumizi Mengineyo | Ruzuku | | Maendeleo | |
| | | | | M/Mengineyo | Mshahara | SMZ | Muhisani |
| **PL0101: Maendeleo ya Kilimo** | **65,555,672,000** | **5,949,523,402** | **1,317,845,810** | **2,745,050,000** | **8,530,650,000** | **20,200,000,000** | **26,812,602,788** |
| SL010101: Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji *(00000P001: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji)* | 7,921,737,000 | 1,548,519,397 | 566,999,815 | | | | 5,806,217,788 |
| *00000P032: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula* | 12,500,000,000 | | | | | | 12,500,000,000 |
| *00000P034: Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji* | 3,950,000,000 | | | | | 200,000,000 | 3,750,000,000 |
| SL010102: Utafiti na Mafunzo ya Kilimo na Mifugo- ZALRI | 8,353,750,453 | | | 1,440,500,000 | 6,913,250,453 | | |
| SL010103: Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula | 5,151,850,000 | 4,401,004,005 | 750,845,995 | | | | |
| *00000P028: Mradi wa Ukarabati na Ujenzi wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula* | 20,000,000,000 | | | | | 20,000,000,000 | |
| *00000P035: Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na kuhakikisha usalama wa Chakula (STREPHIT)* | 2,365,590,000 | | | | | | 2,365,590,000 |
| *00000P039: Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa kukuza uchumi jumuishi (FAO)* | 1,441,750,000 | | | | | | 1,441,750,000 |
| *00000P040: Mradi wa Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Huduma Endelevu za Ugani wa Kilimo* | 400,000,000 | | | | | | 400,000,000 |
| *00000P041: Mradi wa Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakbali wa Sekta ya Kilimo* | 549,045,000 | | | | | | 549,045,000 |
| SL010105: Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 2,921,949,547 | | | 1,304,550,000 | 1,617,399,547 | | |
| **PL0102: Maendeleo ya Rasilimali za Misitu** | **7,459,898,000** | **2,606,280,680** | **1,433,617,320** | **0** | **0** | **2,000,000,000** | **1,420,000,000** |
| SL010201: Maendeleo na Uhifadhi wa Misitu | 4,039,898,000 | 2,606,280,680 | 1,433,617,320 | | | | |
| *00000P036: Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)* | 100,000,000 | | | | | | 100,000,000 |
| *00000P037: Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi ya Ardhi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR* | 1,200,000,000 | | | | | | 1,200,000,000 |
| *00000P038: Mradi wa Kuimarisha usimamizi wa hifadhi ya akiba ya Ufufuma-Pongwe* | 120,000,000 | | | | | | 120,000,000 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *00000L051: Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanic Garden) na mashamba ya Serikali* | 2,000,000,000 | | | | | 2,000,000,000 | |
| **PL0103: Maendeleo ya Mifugo** | **11,463,099,000** | **3,016,031,768** | **697,067,232** | **0** | **0** | **2,500,000,000** | **5,250,000,000** |
| SL010301: Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo | 3,713,099,000 | 3,016,031,768 | 697,067,232 | | | | |
| *00000P029: Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu* | 2,500,000,000 | | | | | 2,500,000,000 | |
| *00000P033: Programu ya Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa wafugaji wadogo (C-SDTP)* | 5,250,000,000 | | | | | | 5,250,000,000 |
| SL010303: Taasisi ya Utafiti wa Mifugo | 0 | | | 0 | 0 | | |
| **PL0105: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo** | **8,249,434,000** | **6,446,048,217** | **1,803,385,783** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| SL010501: Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 2,909,287,000 | 1,859,286,568 | 1,050,000,432 | | | | |
| SL010502: Mipango Sera na Utafiti wa Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 739,426,000 | 384,426,456 | 354,999,544 | | | | |
| SL010503: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo - Pemba | 4,600,721,000 | 4,202,335,193 | 398,385,807 | | | | |
| **JUMLA KUU** | **92,728,103,000** | **18,017,884,067** | **5,251,916,145** | **2,745,050,000** | **8,530,650,000** | **24,700,000,000** | **33,482,602,788** |

**Kiambatanisho Nam. 7A: Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliajimaji**

**Kwa mwaka wa fedha 2024/2025** Mradi huu umeombewa TZS bilioni 24.500 ambapo TZS milioni 500.000 kutoka SMZ na TZS bilioni 24.000 kutoka EXIM BANK ya Korea. Hadi kufikia Machi 2025 mradi umepata TZS bilioni 15.355 kutoka EXIM BANK ya Korea na TZS milioni 364.000 kutoka SMZ.

**Malengo kwa Mwaka 2024/2025**

i. Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagliaji yenye ukubwa wa eneo la hekta 131 katika bonde la Cheju B';
ii. Ujenzi wa mitaro midogo yenye urefu wa Kilomita 20 kwa kiwango cha saruji katika mabonde ya Kilombero, Cheju na Kinyasini;
iii. iii.Ununuzi wa mitambo midogo ya kusaidia kazi za kilimo, palizi na uvunaji katika mobende ya umwagiliaji; na
iv. Kusimamia maeneo yalitojengwa miundombinu ya umwagiliaji maji.

**Utekelezaji wa Malengo**

i. Kazi za uchimbaji wa misingi mikubwa na midogo ya kutolea maji ya ziada (Primary, Secondary and Tertiary Drainage Canals) katika bonde la Cheju B zimekamilika ambapo misingi yenye urefu wa kilometa 5 zimekamilika kwa asilimia 100.
ii. Kazi za ujenzi wa misingi ya ndani ya saruji (Tertiary Irrigation canals) katika mabonde yote ya Mradi imekamilika ambapo misingi yenye urefu wa kilometa 20 imekamilika kwa asilimia 100.
iii. Katika kufimamia miundombinu ya umwagiliaji iliyojengwa wizara imekamilisha ujenzi wa uzio katika bonde la kinyasini wenye urefu wa mita 300.
iv. Ujenzi wa Ofisi katika mabonde 6 ya Mradi (Cheju, Kilombero, Mlemele, Kibokwa, Kinyasini na Chaani) zimekamilika.

**Gharama za mradi:** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu unaombewa TZS bilioni 5.806 kutoka kwa wahisani EXIM BANK ya Korea. Utekelezaji halisi umekamilika, hivyo fedha hizi ni kwa ajili ya kulipia madeni ya watekelezaji baada ya kukamilisha utekelezaji kwa mujibu wa mikataba yao.

**Shabaha za 2025/2026**

i. Kukamilisha malipo kwa kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagliaji yenye katika bonde la Cheju B';
ii. Kukamilisha ununuzi wa mitambo midogo ya kusaidia kazi za kilimo, palizi na uvunaji katika mobende ya umwagiliaji; na
iii. Kusimamia maeneo yalitojengwa miundombinu ya umwagiliaji maji.

**Kiambatanisho Nam 7B: Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2024/2025** Mradi huu ulipangiwa kiasi cha TZS bilioni 22.500 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. Hadi kufikia Machi 2025 mradi umepata TZS milioni 330,345,539 kutoka SMZ. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kukarabati maghala na ununuzi wa chakula |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:** Kuhakikisha haki ya upatikanaji wa chakula katika ngazi ya kaya na taifa inafikiwa. |
| **Malengo ya mwaka 2024/2025**<br>i. Kumalizia ukarabati wa maghala<br>ii. Kununua na kuijengea mitambo ya baridi katika maghala.<br>iii. Kununua chakula cha akiba |
| **Kazi zilizotekelezwa 2024/2025**<br>i. Kazi za ukarabati wa maghala mawili ya Njiwa wengi na New Ferry Malindi zimekamilika.<br>ii. Mchakato wa ukarabati wa maghala 6 kwa upande wa pemba na 3 unguja umekamilika na mkandarasi ameshakabidhiwa kwaajili ya kuanza kazi.<br>iii. Kazi ya ujenzi wa vihenge haijaanza, inasubiriwa kutekelezwa kwa agizo la Mh. Rais la kufanya wasilisho la Mpango wa Biashara wa mradi husika kwa Serikali.<br>iv. MoU baina ya Wizara ya Kilimo na NFRA kwa ajili ya ununuzi wa nafaka tayari imeshakamilika na kusainiwa pande zote. |
| **Kwa mwaka 2025/2026:** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 20 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. |
| **Kazi zilizopangwa 2025/2026**<br>i. Kumalizia ukarabati wa maghala<br>ii. Kununua na kuijengea mitambo ya baridi katika maghala.<br>iii. Kununua chakula cha akiba |

**Kiambatanisho Nam 7C: Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi (Kaskaizini Unguja na Kaskazini Pemba)**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 1.442 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**FAO, ILO,UNCDF,UNIDO,UN Women)**. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kubadili mifumo ya chakula ili kuchochea Uchumi jumuishi, na kuongeza usalama wa chakula na lishe nchini |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:**<br>i. Kuimarisha minyororo ya thamani ya mazao ya chakula (migomba na mihogo) na mwani kwa kutumia mbinu jumuishi na zinazokabiliana na mabadiliko ya tabia nchi; na<br>ii. Kuongeza ujuzi na uwezo wa vijana na wanawake katika kujiajili na kufikia fursa mbali kwenye sekta kilimo na miradi ya kijamii. |
| **Malengo ya mwaka 2025/2026**<br>i. Kusaidia wakulima upatikanaji wa mbinu mbali mbali zinazoendana na mabadiliko ya tabia nchi mfano miundombinu ya umwagiliaji na uzalishaji wa vifaa uzalishaji mazao ya Bahari kwa kuchanganya na hasa mwenye maji ya kina kirefu na hii itapelekea upatikanaji wa aina tofauti za vyakula na kipato;<br>ii. Kuimarisha mbinu bora za uhifadhi wa mazao ili kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, kusaidia mbinu mbali mbali za usarifu wa mazao, kuongeza thamani, upatikanaji wa masoko na kuongeza uwezo wa ushindani kibiashara;<br>iii. Kushajihisha teknolojia za kidijitali ili kusaidia uundaji na urasimishaji wa vikundi na vyama vya ushirika; na<br>iv. kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo ya utoaji mikopo nafuu, pembejeo na teknolojia. |
| **Shabaha za mwaka 2025/2026**<br>i. Kuanzisha mashamba 8 ya uzalishaji wa mbegu za mihogo yenye ukubwa wa ekari 1;<br>ii. Kutoa taaluma ya kilimo himilivu na kujengea uwezo kaya 300 katika kampeni ya uzalishaji bora wa zao la migomba;<br>iii. Kuanzisha mashamba 30 yanayomilikiwa na wakulima 30 ya uzalishaji kibiashara ya mazao ya migomba na mihogo;<br>iv. Kujengea uwezo wanawake 100 na vijana150 katika kilimo mchanganyiko cha mazao ya Bahari;<br>v. Kujengea uwezo wakulima 1000 (600 wanawake, 400 wanaume) huduma za ugani kidijitali na maswala ya kijinsia;<br>vi. Kujengea uwezo wa kitaasisi vikundi 40 vya uzalishaji; na<br>vii. Kujengea uwezo na kuviendeleza vikundi 5 vinavyojishughulisha na usarifu wa mazao wa zao la mwani. |
| **Kazi zilizopangwa 2025/2026**<br>i. Kununua vifaa vya umwagiliaji na uzalishaji wamazao ya Bahari kwa kuchanganya na hasa mwenye maji ya kina kirefu;<br>ii. Kuanzisha mashamba ya mfano ya uzalishaji kibiashara kwa kutumia dhana ya shamba darasa inayozingatia na uendeshaji wa Pamoja kwa kuzingatia maswala mbali mbali ya mgawanyo wa majukumu kwa jamii husika yakiwemo makundi |

mbalimbaliKununua na kuijengea mitambo ya baridi katika maghala;

iii. Kuanzisha mashaba ya ya kibiashara ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mihogo;

iv. Kutoa taaluma uhifadhi wa mazo, uongezaji wa thamani, ubora wa bidhaa na utafutaji wa masoko; na

v. Kutengeneza mpango mkakati wa zao la mwani na kushauri muundo wa kitaasisi.

**Kiambatanisho Nam. 7D: Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania – Kilimo P4R**

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha **2024/2025** mradi huu umetengewa jumla ya TZS bilioni 18.750 chini ya udhamini wa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Hadi kufikia **Machi 2025** mradi umetumia **TZS bilioni 2.07 (20%).** |
| **Malengo ya Mradi:**<br>i. Kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi; na<br>ii. Kuimarisha uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula. |
| **Maeneo Makuu ya Mradi:**<br>i. Kuongeza utoaji wa huduma za utafiti, mbegu na ugani<br>ii. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde manane (8); na<br>iii. Kufanya uratibu wa shughuli za Mradi. |
| **Shabaha kwa mwaka 2024/2025**<br>i. Kufanya ukarabati wa majengo wa maabara za ZARI za Kizimbani na Matangatuani;<br>ii. Kuendeleza tafiti za mazao ya mpunga, muhogo, ndizi na tungule;<br>iii. Kufanya utafiti wa afya ya udongo;<br>iv. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya mashamba ya mbegu yaliyopo Bambi, Kibondemzungu, Mwera, Kizimbani na Ole;<br>v. Kufanya ukarabati wa vituo vinne vya huduma za wakulima katika mashamba ya Bumbwisudi (2), Mtwango (1) na Kibokwa (1);<br>vi. Kufundisha maofisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari;<br>vii. Kufundisha wakulima njia bora za kilimo kwa kutumia teknolojia, kilimo biashara na udhibiti wa upotevu wa mazao baada ya mavuno;<br>viii. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji hekari 434 katika mabonde 8 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kibokwa, Mwera, Makombeni, Weni, Saninga na Kinyakuzi. Ukarabati utahusisha njia za kupitishia maji, kuchimba visima, njia za ndani nakadhalika;<br>ix. Kununua vifaa kwa ajili ya kuwafundishia vijana kutoa huduma mashambani, vifaa hivyo ni, trekta ndogondogo za kulimia, kupandia, kupalilia na kuvunia. |
| **Kazi zilizotekelezwa 2024/2025**<br>i. Mkataba wa kusarifu michoro ya majengo ya maabara umesainiwa na unategemewa kukamilika mwezi Mei, 2025;<br>ii. Tafiti tatu za kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi zinaendelea. Shughuli hii ni endelevu;<br>iii. Hatua ya kupeleka sampuli za udongo kwenye maabara ya TARI imefanyika na tunasubiri majibu. Shughuli hii ni endelevu na utafiti unaendelea;<br>iv. Mkataba wa kusarifu michoro ya miundombinu ya mbegu umesainiwa na unategemewa kukamilika mwezi Mei, 2025;<br>v. Mkataba wa kusarifu michoro ya vituo umesainiwa na unategemewa kukamilika mwezi Mei, 2025;<br>vi. Vifaa vya teknolojia ya habari vimenunuliwa, mafunzo yanasubiri uwepo wa mfumo wa kilimo (Kilimo App System), Mkataba wa kutayarisha mfumo wa kilimo |

| |
|---|
| umesainiwa na unategemewa kukamilika mwezi Agosti, 2025;<br>vii. Shughuli hii imetekelezwa kwa kutoa mafunzo kwa wakulima 400 juu ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya kilimo shadidi;<br>viii. Utaratibu wa kumpata Mshauri Elekezi wa kusarifu michoro kwa mabonde 16 unaendelea hatua za mwisho; na<br>ix. Mkataba wa kusambaza (supply) vifaa umesainiwa, na vifaa vinategemewa kuwasilishwa mwezi Mei, 2025. |
| Kwa mwaka **2025/2026**: Mradi huu umepangiwa kiasi cha **TZS bilioni 12.500** Kutoka washirika wa maendeleo Benki ya Dunia. |
| **Kazi zilizopangwa 2025/2026**<br>i. Kutafuta mjenzi na kuanza ukarabati wa majengo ya maabara;<br>ii. Kuendeleza tafiti za kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi;<br>iii. Kutafuta mjenzi na kuanza ukarabati wa miundombinu ya mbegu;<br>iv. Kutafuta mjenzi na kuanza ukarabati wa vituo vya huduma kwa wakulima;<br>v. Kufundisha maofisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari;<br>vi. Kutoa kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya kilimo shadidi;<br>vii. Kukamilisha usarifu wa michoro kwa mabonde 16; kutafuta wajenzi na kuanza ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 10 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kianga, Kibokwa, Mwera, Makombeni, Tibirinzi, Weni, Saninga na Kinyakuzi; na<br>viii. Kuwafundishia vijana kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo. |

**Kiambatanisho Nam. 7E: Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa kuongeza tija na Uzalishaji kupitia huduma za kisasa za kilimo katika umwagiliaji**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2024/2025:** Mradi umepangiwa kiasi cha **TZS bilioni 1.5** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo – Serikali ya Korea. Hadi kufika Machi 2025 mradi haukupata fedha kutokana na changamoto za kimkataba ambazo kwa sasa zimesawazishwa. |
| **Malengo ya Mradi**<br>i. Kuchangia uimarishaji wa uhakika wa chakula na kuongeza kiwango cha kipato cha wakulima wa mpunga Zanzibar; na<br>ii. Kuongeza tija ya mpunga katika mashamba ya umwagiliaji. |
| **Shabaha kwa mwaka 2025/2026**<br>i. Kununua matrekta ya kilimo katika mabonde ya mradi wa Umwagiliaji kwa ajili ya jumuiya za wakulima kwa kuimarisha zao la mpunga;<br>ii. Kununua matrekta, na machine ya kuvunia mpunga kwa ajili ya Taasisi ya Huduma za zana za kilimo kwa kutolea mafunzo kwa jumuiya za wakulima wa mpunga;<br>iii. Kuboresha miundombinu ya kilimo kwa kutengeneza njia za mashambani, vivukio vya matrekta pamoja na maeneo ya kuanikia mpunga;<br>iv. Kujenga maeneo ya kuhifadhia mazao ya mfunga, matrekta, pamoja na uchimbaji wa kisima katika kuongeza upatikanaji wa maji mengi bonde la Chaani<br>v. Kununua vifaa vya usimamizi na ufuatiliaji wa vyanzovya maji katika maeneo ya umwagiliaji maji. |
| **Kwa mwaka 2025/2026:** Mradi umepangiwa kiasi cha TZS bilioni **3.950** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo - Umoja wa Nchi za Ulaya |

**Kiambatanisho Nam. 7F: Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Hifadhi ya Akiba ya Ufufuma-Pongwe**

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Mradi huu umetengewa jumla ya TZS 120,000,000 (Fedha hizo zinasimamiwa na Jumuiya ya WCS). |
| **Malengo ya mwaka 2025/2026**<br>Kutengeneza na kutenga Hifadhi mpya ya msitu ili kuunganisha Hifadhi ya Msitu ya Kiwengwa Pongwe na Hifadhi ya Taifa Jozani Ghuba ya Chwaka na Hifadhi hai. |
| **Maeneo Makuu ya Mradi:** Mkoa wa Kusini Unguja - Wilaya ya Kati (Shehia nane (8) zilizopo wilaya ya Kati ikijumuisha Jendele, Umbuji, Pagali, Bambi, Pongwe, Uroa, Marumbi na Chwaka. Kwa ujumla Msitu huo una ukubwa wa hekta 1988. |
| **Malengo makhsusi ya mradi:**<br>i. Kuwaunganisha na kuwalinda Wanyama adimu na wakipekee ambao wanapatikana katika hifadhi mbili;<br>ii. Kuongeza mapato yatokanayo na rasilimali za Misitu kwa Shehia za mradi;<br>iii. Kutangazwa rasmi kwa hekta 1,988 za msitu zinazounda kiunganishi kati ya hifadhi za Jozani na Kiwengwa;<br>iv. Kuimarisha usimamizi wa hekta 1,988 za msitu jrani na hifadhi za Jozani na Kiwengwa; na<br>**v.** Kuongeza alama za vipimo vya ufuatiliaji wa usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa (METT). |
| **Shabaha kwa mwaka 2025/2026**<br>i. Kuandaa ramani za eneo pendekezwa na kuutambulisha mradi kwa wadau;<br>ii. Kufanya Mapitio ya CoFMA na kuzitangaza katika gazeti rasmi lla Serikali;<br>iii. Kufanya mapitio ya azma na kuitangaza hifadhi (Final order);<br>iv. Kutoa elimu ya uhifadhi na usimamizi shirikishi kwa jamii, ikiwemo wanafunzi; na<br>v. Kuandaa mfumo wa kuweka kumbukumbu ya malalamiko na kero za wanajamii. |

**Kiambatanisho Nam. 7G: Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC)**

| |
|---|
| **Kwa mwaka wa fedha 2024/2025,** mradi ulitengewa kiasi cha TZS milioni **500.000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo – Umoja wa Ulaya. Hadi kufikia Machi 2025 Mradi umeingiziwa TZS milioni **312** sawa na asilimia **62.4** |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha mchango wa sekta ya ufugaji nyuki katika ukuaji wa uchumi shirikishi nchini Tanzania |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:** Kuiwezesha asali bora inayozalishwa kwa njia endelevu ya mazingira kupenya katika masoko. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2024/2025**<br>i. Kufanya Mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Misitu (1996);<br>ii. Kuimarisha Skuli ya Kilimo (SOA) ili kuweza kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki;<br>iii. Kuendelea na tafiti za nyuki;<br>iv. Kutoa mafunzo ya Ufugaji Bora wa Nyuki;<br>v. Kuendeleza upatikanaji wa pembejeo za ufugaji nyuki; na<br>vi. Kujenga Kituo cha Mauzo ya Bidhaa za Nyuki. |
| **Utekelezaji 2024/2025**<br>i. Rasimu ya Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali Misitu (2025) imetengenezwa na wataalamu wa sekta ya Maliasili kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu;<br>ii. Manzuki Darasa kwa ajili ya mafunzo ya ufugaji nyuki imejengwa na kuanza kutumika katika Skuli ya Kilimo – Kizimbani. Aidha, wakufunzi wawili (2) wa SOA wamepatiwa mafunzo ya Utalii wa Nyuki (Api tourism). Hii ni muendelezo wa kuimarisha taasisi za elimu na utoaji wa elimu ya ugani kwa wafugaji nyuki wa Zanzibar;<br>iii. Muongozo wa Ufundishaji (Training Manual) wa Somo la Ufugaji Nyuki (Principles of Beekeeping - PS 2406) umetayarishwa na kuwasilishwa katika Kamati ya Uongozi ya Chuo;<br>iv. Utafiti wa wadudu vamizi na waharibifu katika ufugaji nyuki imefanyika kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI);<br>v. Wafugaji nyuki 754 (wanaume 424, wanawake 330) wamepatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki bora kutoka kwa maafisa misitu wa wilaya 4 za Pemba. Hii ni muendelezo wa kufundisha wafugaji nyuki 1,000 kisiwani Pemba;<br>vi. Mafundi nguo 30 wamepatiwa mafunzo ya ushonaji mavazi kinga ya nyuki katika vituo vya Mafunzo ya Amali Daya na Vitongoji. Hii ni muendelezo wa kuimarisha upatikanaji wa vifaa na nyenzo za kufugia nyuki kwa wafugaji nyuki kisiwani Pemba; na<br>vii. Mizinga ya kufugia nyuki 200 imetolewa kwa vikundi 23 vya wafugaji nyuki. Vikundi 6 Wete, 5 Micheweni, 7 Chake Chake na 5 Mkoani. |

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, mradi umetengewa kiasi cha TZS milioni 100 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo – Umoja wa Ulaya. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa**<br>i. Kutoa mafunzo ya nyuki;<br>ii. Kuendeleza upatikanaji wa pembejeo za ufugaji nyuki;<br>iii. Kuanzisha na kuendeleza Hifadhi za Nyuki katika Misitu ya Jamii |

**Kiambatanisho Nam. 7H: Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2024/2025** Mradi huu ulipangiwa kiasi cha TZS Bilioni **2.000** kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. Hadi kufika Machi 2025 mradi huu umeingiziwa **TZS 149,520,620** kwa utekelezaji. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuimarisha mazingira ya chinjio na karantini; kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen kwa ajili ya kuhifadhia mbegu za madume wa ng'ombe; kuimarisha miundombinu ya utafiti wa Mifugo na kudhibiti ndege waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru); pamoja na kuimarisha maudhui ya Kilimo TV. |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:**<br>i. Kuimarisha miundo mbinu ya mifugo kwa kutoa huduma bora kwa jamii za wafugaji na wakulima;<br>ii. Kutoa elimu, teknolojia na mbinu bora za kilimo kwa wakulima kupitia maudhui ya TV; na<br>iii. Kutambua maeneo yenye makundi makubwa ya kunguru na kutekeleza shughuli za kuangamiza kunguru katika maeneo yaliyopewa kipaumbele. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2024/2025**<br>i. Kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen;<br>ii. Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba;<br>iii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti Kizimbani – maabara, mabanda ya mbuzi na ofisi; na<br>iv. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti wa mifugo Chamanangwe, Pemba ikiwemo maabara ndogo ya mifugo, mabanda ya utafiti ya kuku na mbuzi. |
| **Kazi zilizotekelezwa:**<br>i. Fedha za awali asilimia 20 zimeshaingizwa kwa ajili ya msambazaji wa mtambo, pia eneo la kuwekea mtambo tayari limeshafanyiwa ukarabati;<br>ii. Mkandarasi ameshakabidhiwa kazi ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba kwaajili ya kuanza kazi;<br>iii. Kazi ya ujenzi wa maabara ya utafiti wa magonjwa ya Wanyama kisiwani Unguja umeshaanza na unaendelea;<br>iv. Kazi ya ujenzi wa banda la utafiti wa mbuzi kisiwani Unguja umeshaanza na unaendelea; na<br>v. Kazi ya ujenzi wa maabara ya utafiti wa magonjwa ya Wanyama Pamoja na mabanda ya utafiti wa kuku na mbuzi kisiwani Pemba uko katika hatua ya usanifu |

| |
|---|
| wa michoro. |
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS Bilioni **2.500** kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2025/2026**<br>i. Kununua mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrogen;<br>ii. Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba;<br>iii. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti Kizimbani – maabara, mabanda ya mbuzi na ofisi;<br>iv. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti wa mifugo Kizimbani Unguja ikiwamo – maabara ya utafiti wa magonjwa ya wanyama, mabanda ya utafiti wa mbuzi na kondoo;<br>v. Ujenzi wa miundombinu ya utafiti wa mifugnangwe Pemba ikiwamo – maabara ya utafiti wa magonjwa ya wanyama, mabanda ya utafiti wa mbuzi na kondoo na mabanda ya utafiti wa kuku;<br>vi. Kudhibiti Wanyama waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru);<br>vii. Kuzindua na kuimarisha maudhui ya Kilimo TV;<br>viii. Kufanya utambuzi wa kina kwa lengo la kubaini maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa kunguru ,viota na mabadiliko ya tabia zao; na<br>ix. Kutengeneza na kuweka mitego kwa ajili ya kuwakamata kunguru katika maeneo yenye yaliopendekezwa. |

**Kiambatanisho Nam. 7I: Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha usalama wa chakula (STREPHIT)**

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi huu umetengewa jumla ya TZS bilioni **4.08.** Hadi kufika Machi 2025 mradi huu umeingiziwa **TZS 40,000,000** kwa utekelezaji. |
| **Malengo kwa Mwaka 2024/2025** |
| i. Kuongeza upatikanaji mazao ya Kilimo yaliyosalama na bora kwa masoko ya Kitaifa na Kimataifa;<br>ii. Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa udhibiti rasmi wa uingizaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo; na<br>iii. Huduma za Kitaifa za Afya ya Mimea kutumia ufuatiliaji unaoaminika na mifumo ya ulinzi wa mimea. |
| **Shabaha za Mradi:**<br>i. Kufanyika kwa warsha ya siku mbili ambayo imezungumzia masuala mazima ya uandaaji wa mtaala mpya kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wanaojishughulisha na utoaji wa huduma za afya ya mimea nchini amapo washiriki waligusia maeneo yote muhimu yanayogusa tasnia nzima ya huduma za afya ya mimea;<br>ii. Kuanzisha kwa mfumo wa utoaji wa cheti cha usafi wa mimea kwa njia ya mtandao (ATMIS) ambapo malipo ya yatakuwa chini ya mfumo wa Zanmalipo;<br>iii. Uandaaji wa Kitabu cha agizo la uingizaji wa bidhaa ndani ya mfumo wa utoaji cheti cha usafi wa mimea kwa njia ya mtandao (IMPORT ORDER BOOK-ATMIS);<br>iv. Kununua Kombo Tool Box kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa utoaji wa taarifa za wadudu, maradhi ya mimea na mazao yanayoingia na kutoka nchini;<br>v. Kushajihisha Mpango wa utafiti utakaoeleza uundaji wa orodha ya wadudu nchini;<br>vi. Kukarabatiwa kwa maabara na za wadudu Unguja na Pemba na kujengewa uwezo kwa wataalamu watakaoendesha shughuli za maabara hizo;<br>vii. Kusaidia katika utayarishaji wa Sheria na Kanuni za Zanzibar; na<br>viii. Kusaidia utayarishaji upya wa muundo wa URT-NPPO katika Shirika la Kimataifa la masuala ya Ulinzi wa mimea (IPPC). |
| **Kazi zilizotekelezwa:**<br>i. Kufanya mapitio ya Project Log frame, ya mradi wa STREPHIT kupitia taarifa za baseline survey na tathmini na ufuatiliaji;<br>ii. Kufanyika kwa warsha ya tathmini na udhibiti wa Ugonjwa wa Shada ya Migomba (Banana Bunchy Top Virus (BBTV); na<br>**iii.** Kufanyika kwa warsha ya mapitio ya rasimu ya kanuni za afya ya mimea za Zanzibar. |
| **Kwa mwaka 2025/2026:** mradi umetengewa kiasi cha TZS blioni 2.366 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |
| **Kazi zilizopangwa kutekelezwa 2025/2026**<br>i. Kukamilishwa kwa rasimu ya kanuni za Afya ya mimea Zanzibar<br>ii. Kukamilishwa ujenzi wa maabara kuu za afya ya mimea katika afisi za Kitengo cha |

Utibabu na Ukaguzi wa Mazao, Unguja na Pemba

iii. Kukamilishwa ujenzi wa maabara ndogo katika afisi za kitengo cha Utibabu wa Mimea na Ukaguzi Mazao Bandarini Malindi

iv. Kukamilishwa ujenzi wa maabara za ndogo za Kontena (Kontena minilabs) katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume, bandari ya Mkoani Pemba na bandari ya Wete

v. Kuwajengea uwezo watumishi wa Kitengo cha utibabu wa mimea na ukaguzi wa mazao kwa lengo la kukizi vigezo vya kimataifa vinavyohusiana na afya ya mimea

vi. Kuimarisha matumizi ya mfumo wa utoaji vibali vya afya ya mimea wa e - kilimo

vii. Kuanzishwa kwa mkakati wa udhibiti wa maradhi ya migomba hususani Banana Bunch Top Virus (BBTV)

viii. Kuwajengea uwezo marubani wa drone wa juu ya namna ya kufanya upembuzi wa taarifa (analysis of multispectral data) zilizopatikana kwa kutumia drone

ix. Kukamilisha manunuzi ya gari na pikipiki kwa ajili ya kuboresha shughuli za afya ya mimea

**Kiambatanisho Nam. 7J: Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejesheaji wa ardhi - FOLUR**

| |
|---|
| **Gharama za mradi:** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi huu umetengewa jumla ya TZS milioni 682.800 kutoka Global Environmental Facility **(GEF).** Hadi kufikia Machi 2025 mradi umeingiziwa jumla ya TZS milioni 500.000 |
| **Malengo kwa Mwaka 2024/2025** |
| i. Uhifadhi wa Misitu katika maeneo ya Kaskazini A na B; na<br>ii. Kushirikisha sekta za Kilimo, Mazingira, Ardhi na sekta nyengine zenye mnanasaba na Uhifadhi wa Misitu katika kuhifadhi na kusimamia rasilimali hiyo. |
| **Shabaha za Mradi:**<br>i. Kukarabati majengo ya ofisi;<br>ii. Kuhamasisha jamii zinazozunguka Wilaya za Kaskazini A na B; na<br>iii. Kutoa elimu ya Uhifadhi. |
| **Kazi zilizotekelezwa**<br>i. Kazi ya ukarabati wa jengo moja la ofisi inaendelea ambapo ukarabati umefikia asilimia 80%; na<br>**ii.** Vikundi 10 vya wanajamii vimepewa elimu juu ya uhifadhi wa rasilimali za misitu. |
| **Kwa mwaka 2025/2026:** mradi umetengewa kiasi cha TZS bilioni 1.200 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |

**Kiambatanisho Nam. 7K: Mradi wa Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unaozingatia Mabadiliko ya Tabianchi**

| |
|---|
| Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Mradi huu umetengewa jumla ya TZS **bilioni 7.500** Mkopo kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo IFAD na OPEC. Hadi kufikia Machi 2025 mradi haukupata fedha kutokana na kuchelewa kukmilisha taratibu za kimkataba. |
| **Malengo ya Mradi**<br>i. Kuchangia katika kuleta mageuzi kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa maziwa kwa ajili ya kukuza hali hali ya mazisha kwa jamii, kuongeza uhakika wa chakula na vilevile kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi katika sekta ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa; na<br>ii. Kukuza kipato, uhimilivu wa tabia nchi, kuongeza lishe kwa wazalishaji wadogowadogo wa maziwa na ushiriki wao kikamilifu na bora katika mnyonyoro wa thamani wa maziwa. |
| **Maeneo Makuu ya Mradi**<br>i. Mpango wa uzalishaji wa maziwa wenye tija na himilivu; na<br>ii. Ushirikishwaji katika minyonyoro bora ya thamani, uwekezaji binafsi, unywaji wa maziwa na pamoja na sera. |
| **Shabaha kwa mwaka 2025/2026**<br>i. Uanzishaji wa vituo vidogo vya ukusanyaji wa maziwa katika maeneo maalum;<br>ii. Ukarabati wa vituo vya ukusanyaji na usarifu wa maziwana (MCCs) viliopo na ujenzi wa vituo vingine vipya;<br>iii. Ununuzi wa mitamba bora ya ng'ombe wa kisasa wa maziwa;<br>iv. Ujenzi wa viwanda vidogo vya kusarifu maziwa;<br>v. Ukarabati wa miundombinu ya mashamba ya mbegu yaliyopo Kizimbani;<br>vi. Kufundisha maofisa ugani kuhusiana namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia bora za kisasa;<br>vii. Kufundisha wafugaji wa ng'ombe wa maziwa njia bora za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuzingatia njia bora za uhimilivu wa tabia nchi; na<br>viii. Kuendeleza ujenzi wa mitambo ya biogas Unguja na Pemba kwa lengo la upatikanaji wa nishati ya kupikia na mbolea bora kwa ajili ya uzalishaji wa mazao pamoja na malisho ya mifugo. |
| **Kwa mwaka 2025/2026:** mradi umetengewa kiasi cha TZS **bilioni 5.250** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |

**Kiambatanisho Nam 7L: Mradi wa Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Huduma Endelevu za Ugani wa Kilimo**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS milioni 400.000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuwajengea uwezo mabibi na mabwanashamba ili wawe na ubunifu na uwezo wa kuwaelimisha wakulima kwa kutumia mbinu/njia bora za uzalishaji wa mazao kwa wingi kwa kutumia pembejeo zilizopo. |
| **Malengo Makhsusi ya Mradi:**<br>i. Kuwapa mafunzo ya GAP kwa kutumia njia jumuishi na rahisi za teknologia kwa wakulima za kuongeza uzalishaji na kujenga mpango wa mda mrefu wa huduma za ugani nchini;<br>ii. Kuandaa utafiti wa kumjuwa aina ya mkulima, aina ya mazao anayozalisha na alipo ili kujuwa mahitaji ya pembejeo hitajika;<br>iii. Kutumia mbinu shirikishi za kuwaelimisha wakulima kupitia mashamba ya maonyesho (Demo plot) kupiti vikundi na mmkulima moja moja kwa mazao ya Nafaka na jamii ya kunde na kuwaonysha wakulima wengine wasiopata mafunzo na wao waweze kuiga na kuongeza mapato ya uzalishaji;<br>iv. Kuanda mfumo wa upatikanaji taarifa za wakulima na uzalishaji kwa kutumia tekinologia ya Digital plat foum; na<br>v. Kujenga mfumo mzuri wa masoko na mpangilio wa uletaji mazao kulingana na mahitaji ya soko. |
| **Shabaha za mwaka 2025/2026**<br>i. Kumaliza kazi zilizopangwa za mwaka uliopita mwaka wa kwanza ikiwemo kuunda timu ya PMU ya mradi na safu ya utendaji na kununua Extension tools;<br>ii. Kufanya mobilization ya kushirikisha makundi maalum ya vijana na kinamama kwa ajili ya mnyororo wa thamani kwa kupitia Digital plat foum;<br>iii. Kufanya usimamizi wa ujenzi wa kituo ili kiwe kinatumika kutoa taalum; na<br>iv. Kuandaliwa TOR na pamoja na MOU za mradi na wafadhili, pamoja na usimamizi IITA ambao watatoa miongozo. |
| **Kazi zilizopangwa 2025/2026**<br>i. Kufanya sensa ya wakulima na kuwatambua wanapolima, aina ya mazao wanayolima, ukubwa wa eneo, na tathmini ya uzalishaji kwa kila msimu;<br>ii. Kuanzisha Demo plot 446 zenye ukubwa tofauti;<br>iii. Kutoa mafunzo maalum kwa wataalam na wakulima viongozi TOT kuhusiana na uzalishaji wa mazao;<br>iv. Kuandaa mazingira ya upatikanaji wa pembejeo rahisi za kilimo; na<br>v. Kuandaa ujenzi wa kituo cha kupashana taarifa Digital plat foum kwa kufanya maandalizi na upatikanaji wa vifaa stahiki kwa ajili ya kituo. |

**Kiambatanisho Nam 7M: Mradi wa Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakbali wa Sekta ya Kilimo**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS milioni 518.750 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Master Card - AGRA. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuinua kipato cha vijana kupitia kilimo na biashara ya mazao ya Horticulture (Youth enterprenuership for future of Agriculture- YEFFA). Mradi huu unatekelezwa katika mikoa mitatu Tanzania bara, na mikoa yote ya Tanzania Zanzibar. Kusaidia vijana 98,000, hususan wanawake na wale walio kwenye hali ngumu, kupata ajira za kuheshimika na zinazoridhisha katika tasnia ya horticulture Tanzania. |
| **Malengo makhsusi ya mradi**<br>i. Kusaidia kuongeza upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana; na<br>ii. Kuongeza uzalishaji, ustahimilivu na uendelevu wa biashara za kilimo, hususan zinazomilikiwa na vijana. |
| **Maeneo Makuu ya Mradi**<br>Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro upande wa Tanzania bara na mikoa yote upande wa Tanzania Zanzibar. |
| **Shabaha kwa mwaka 2025/2026**<br>i. Kuandikisha vijana 98,000 watakaonufaika na mradi, asiliia 70 ikiwa wanawake;<br>ii. Kuteua na kufunza vijana, hususan wanawake kama wakulima viongozi (village-based advisors);<br>iii. Kuhamasisha ushiriki wa vijana kwenye miradi maalum ya serikali;<br>iv. Kufundisha vijana mbinu bora za kilimo, ikiwemo kilimo cha mboga mboga na uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna;<br>v. Kufundisha vijana kuhusu kilimo biashara; na<br>**vi.** Kuunganisha vijana na taasisi zenye nguvu kama wauza pembejeo na wafanya biashara wakubwa wa bidhaa za mboga mboga wa kitaifa na kimataifa. |

**Kiambatanisho Nam 7N: Mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Mimea (Botanic garden) na Mashamba ya Serikali**

| |
|---|
| **Kwa mwaka 2025/2026** Mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS bilioni 2.00 kutoka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. |
| **Lengo kuu la Mradi:** Kuinua mapato ya Serikali kupitia ada ya wageni wanaotembelea shamba la viungo na bustani ya mimea |
| **Malengo makhsusi ya mradi**<br>i. Kusaidia kuboresha shamba kuwa la kisasa lenye aina nyingi za mimea na mandhari ya kuvutia wageni wengi zaidi; na<br>ii. Kuanzisha bustani ya mimea (botanical garden) kwa ajili ya kuongeza wigo wa vivutio vya kutembelea na kutoa huduma bora. |
| **Shabaha kwa mwaka 2025/2026**<br>i. Kutafuta mshauri elekezi kwa ajili ya ubunifu wa bustani ya mimea;<br>ii. Kuchimba kisima na kuweka miundombinu ya umwagiliaji maji;<br>iii. Kuanzisha vishamba vidogo vidogo vya miti ya viungo na madawa;<br>iv. Kurudisha uoto wa asili na miti adimu na iliyo hatarini kutoweka;<br>v. Kuwajengea uwezo wataalamu kuhusu taaluma ya kutoa huduma za mimea ya viungo na madawa kwa wageni;<br>vi. Kujenga jengo la mapokezi na ofisi ya kutoa huduma za utalii wa viungo (spice tourism) na taarifa za mimea ya viungo na madawa;<br>**vii.** Kuanzisha eneo la huduma za mapumziko, sherehe, tafrija na filamu ili kuvutia wageni wengi zaidi;<br>**viii.** Kuboresha njia za ndani ya shamba, kuweka mabango na kuweka lebo;<br>**ix.** Kuweka geti la kisasa na maegesho ya magari;<br>**x.** Kuanzisha mgahawa wa kienyeji wa chai na kahawa ya kienyeji (traditional tea and coffee shop);<br>**xi.** Kuanzisha tovuti na kuchapicha vipeperushi kwa ajili ya kulitangaza shamba la viungo na bustani pamoja na kurahisisha upatikanaji wa taarifa; na<br>xii. Kuanzisha ulinzi madhubuti kupitia vikosi vya SMZ. |

**Kiambatanisho Nam. 8: Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Programu kwa Mwaka 2025/2026**

